

MUNGU ASIYEBADILIKA

AKITENDA KAZI KATIKA

NJIA ISIYOTARAJIWA



Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

² Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu kwa maombi. Nina furaha sana kuwa pamoja nanyi usiku wa leo. Na jambo la kwanza tunalotaka kufanya sasa ni kuzungumza na Yeye ambaye tumekuja kumwona, Bwana Yesu. Na tuombe.

³ Baba yetu wa Mbinguni, tunahesabu haya kuwa ni majaliwa makubwa ya jinsi hii kuwa katika kanisa hili dogo usiku wa leo, katika utumishi wa Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, Mwokozi wetu. Tunakushukuru sana kwa neema ambayo ametupa, kuimwaga Damu Yake, kusudi sisi, tulio wachafu, tupate kusafishwa na Upatanisho Wake mkuu.

⁴ Tunaomba kwa ajili ya Kanisa la ulimwenguni kote, kila mahali, kwa kila mshiriki, kila mchungaji. Tunaomba hasa kwa ajili ya kanisa hili na mchungaji wake, usiku wa leo, na kundi hili dogo linalopita hapa katika sehemu hii ya mji. Kama washiriki wa Mwili wa Kristo, tunaomba ya kwamba utawabariki, Bwana. Wabariki mashemasi, wadhamini. Na ni majaliwa makubwa sana kuja, usiku wa leo, kushiriki ushirika huu kwa pamoja, Bwana, tulio nao katika msimamo huu wa pamoja katika Kristo.

⁵ Sasa, Bwana, tunaomba ya kwamba Wewe utamwokoa kila mtu hapa ambaye hajaokolewa, usiku wa leo. Pia mponye kila mgonjwa aliye mgonjwa. Na uwajaze kwa Roho Mtakatifu wale wanaoona njaa na kiu kwa ajili ya jambo hilo. Uwepo katika Neno, usiku wa leo, Bwana, na utuoshe kwa maji ya Neno, tunapongojea zaidi. Katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁶ Salamu kwa Ndugu Cyril, na kwa kundi la Bwana linalokaa sehemu hii ya mji. Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo, kushiriki wakati huu wa ushirika pamoja nanyi, rafiki zangu wapendwa. Nami ninaona wengi wamesimama. Tunatumaini tu kwamba hatutachukua muda mrefu sana, Ujumbe mdogo kutoka kwa Bwana, na zaidi sana ni wakati wa kukusanyika pamoja. Nami nadhani nilikutana na ndugu hapo siku zilizopita, mahali fulani. Nami ninajua niliutambua uso wake, lakini jina lake linasikika kama ninalolijua.

⁷ Na kwa hiyo sisi, wote tukiwa jeshi moja kubwa na lenye nguvu la Mungu, tukitembea kiaskari kuelekea kwenye ushindi wa mwisho mwishoni mwa safari. Na kwenu ninyi Wakristo mliopo hapa, mnaosafiri, amani ya Mungu na iwe juu yenu.

⁸ Nami ninatumaini ya kwamba Mungu atalibariki kanisa hili dogo. Na lijaliwe likue likawe kanisa kuu mno hapa, washiriki wote wajazwe na Roho Mtakatifu; na wawe watiifu sana kwa Roho, hivi kwamba dhambi haiwezi hata kuingia milangoni bila kutajwa na Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo aina ya kanisa tunalotarajia, na kujitahidi sana kusudi tulipate. Ninaamini ya kwamba mambo hayo yanawezekana.

⁹ Na sasa inawezekana, pia, ya kwamba kama tutajisalimisha tu kwa Mungu, na kulisikiliza Neno Lake, na kumwamini Yesu kwa moyo wetu wote, ninaamini ya kwamba kutatokea Kanisa ambapo kwamba mambo hayo yatatukia. Ninajua ingekuwa ni shauku ya—ya moyo wa kila mhudumu, kuingia kwenye kanisa ambalo limejazwa sana na Uwepo wa Mungu, na—na kila mtu akiwa katika upatano kamili na Roho, hata hakutakuwako na dhambi, mshiriki mmoja asingeweza kufanya dhambi. Mara walipoingia mle, wangejua vizuri zaidi kuliko kuja mbele ya kanisa hilo, wakiwa na dhambi hiyo maishani mwao. Roho Mtakatifu angeitaja mara moja, papo hapo, na kusema, “*Hii hapa.*” Sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa, enyi marafiki. Hiyo ndiyo aina ya kanisa. Nasi tunajitahidi kulipata hilo, enyi ndugu, sivyo? [Hao ndugu wanasema, “Amina.”—Mh.] Sote tunajitahidi kupata kitu hicho, na tunatumainia na kuamini.

¹⁰ Na kusudi langu hapa Phoenix ni kuwa pamoja na Wafanyabiashara Wakristo kwenye mkutano huu. Walikuwa ni wakarimu sana, Ndugu Williams hapa, kulitembelea kundi hili zuri la ndugu, kwenye madhehebu mbalimbali, na kadhalika. Na makanisa madogo kote humu nchini, na ninyi ndugu, mlifanya vizuri sana kunialika, kufanya ushirika huu pamoja nanyi. Ninafurahia jambo hilo sana, kwa maana mimi kweli ninapenda ushirika na ndugu zangu. Nafikiri Yesu alisema, “Hivyo ndivyo watu wote watakavyojua kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu,” mwajua, wakati—wakati upendo Wake unashiriki mmoja kwa mwingine.

¹¹ Tumekuwa na siku tatu usiku sasa. Na jana usiku tulikuwa kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, na tulikuwa na wakati mzuri sana kule, na juu kule Tempe. Na halafu hapa kwenye... Nimegeuzwa, nami sijui niko wapi. Hapa, mahali fulani, tulikuwa huko ma—magharibi ya Phoenix, usiku wa kwanza. Na kesho asubuhi, nafikiri, kwenye saa nne, tutakuwa kwa Ndugu Fuller.

¹² Na kesho usiku ni kwenye Hekalu la Imani kwenye Barabara ya Kihindi, ninaamini, ama Barabara ya Shule ya Kihindi, ama kitu kama hicho. Nimechanganyikiwa kabisa. Ni kitu

gani? [Mtu fulani anasema, “Barabara ya McDowell.”—Mh.] Ati McDowell? [“Barabara ya McDowell.”] Barabara ya McDowell. Ile Maskani ya Imani kwenye Barabara ya McDowell. Loo, jamani! Barabara ya Shule ya Kihindi. Hilo si ni jambo la kufurahisha? Ni Kalvari...? [“Maskani ya Ushirika.”] Maskani ya Ushirika. Nimechanganyikiwa kabisa. Nilimsikia Billy akiniambia, tukitoka nje, sasa hivi, “Maskani ya Ushirika.”

¹³ Na, lakini sasa, ninyi watu kwenye ninii yenu... hapa kwenye wajibu wenu, ni kesho asubuhi na kesho usiku. Kumbukeni jambo hilo. Tuko hapa tu matembezini. Hatutaki mhame-hame kutoka kanisa moja hadi jingine. Tutakutana sisi kwa sisi wakati mwingine juma lijalo tena, unaona, na kufanya ushirika pamoja. Lakini wajibu wako uko kwenye kanisa lako. Ninaamini kila Mkristo anapaswa kusimama kwenye wajibu wake wakati huo.

¹⁴ Kwa hiyo nilikuwa nikizungumza na ndugu mmoja hapa leo, Ndugu Sharritt, rafiki wa thamani wa sisi sote, ambaye sote tunamjua, John Sharritt, mtu mu—muungwana tu. Naye alisema, “Ndugu Branham, mara nyingi nilikusikia ukisema ulikuwa unakuja Magharibi siku moja, kuishi.”

¹⁵ Nami nikasema, “Naam, kifungo cha mwisho kinachonifunga na mashariki kimeondolewa sasa: mama yangu. Naye alienda nyumbani kuwa pamoja na Yesu, siku chache zilizopita. Na mama ya mke wangu ameaga dunia pia.”

¹⁶ Kwa hiyo ni kweli, tunatafuta mahali pa kutulia. Na—na kama ikitokea kwamba tushukie huku Tucson, Phoenix, Bwana akituongoza huku, nisingetaka kamwe kuanzisha kanisa. La, bwana. Nisingefanya jambo hilo. Lakini ningeninii... Mimi ni mmishenari. Ndipo wakati nikiwa nimekuja, ninapenda kwenda kutoka kanisa hadi kanisa, kukiweko na ushirika wa namna hiyo. Na kuwa na...

¹⁷ Nafikiri mna makanisa mazuri hapa. Nasi tunaninii tu... Tuna makanisa mengi sana. Inatupasa tu kuyabeba, na kuyajaza. Hivyo tu. Hilo ndilo tunalohitaji. Naam. Tunaninii tu—tunafanya hivyo tu, maana mtu anapoanzisha kanisa jipya, kama lipo mahali popote lilipo, basi, mnaona, halina budi kuvuta kidogo hapa na pale. Wala si—si vizuri kufanya hivyo.

¹⁸ Kwa hiyo kama Bwana angeniongoza, ninawataka ndugu wajue ya kwamba isingekuwa ni kwa ajili ya kanisa lingine. Nisingefanya jambo hilo kamwe, hata kidogo. Mnaona? Ingekuwa tu ni kuja hapa na kushirikiana na kila mmoja wenu, kila mmoja, na kuwa na wakati mzuri sana katika Bwana.

¹⁹ Sasa, basi, msisahau Wafanyabiashara, Wafanyabiashara wa Full Gospel. Watu hawa wanatoka kwenye makanisa yenu yote. Na ushirika huo unaanza Alhamisi ijayo jioni, nadhani. Hiyo ni kweli, Ndugu Williams? Kwenye, huko Ramada mashariki mwa Barabara ya Van Buren. Na sasa, kutakuwako na wahubiri

mashuhuri humo ndani wanaokuja kwenye mkutano huu. Na—nami bila shaka ninataka kuuhudhuria, mimi mwenyewe, kuwasikia hao watu. Ndugu Velmer Gardner, ni mmoja wao, ambaye ni mhubiri hodari sana, na ndugu wengine wengi. Baadhi ya hao wafanyabiashara ambao sijapata kuwasikia bado, wanasema hao ni wahubiri wazuri sana. Nami nina furaha sana kuwasikia, ama nafasi ya kuwasikiliza. Kwa hiyo tunatarajia kukutana nanyi nyote kule.

²⁰ Halafu basi, Bwana akipenda, nafikiri, kama ikipangika namna hiyo, ninakusudiwa kuchukua kiamshakinywa cha Jumamosi asubuhi, na kuhubiri kwenye kiamshakinywa hicho. Halafu basi, ninaamini, alasiri ya Jumapili ifuatayo, kwenye mkutano wa alasiri. Nami natumaini kukutana nanyi kule basi, ninyi nyote watu wa thamani.

²¹ Sasa, sitaki kuwasimamisha kwa muda mrefu sana, maana mtatoka mapema usiku wa leo. Maana, tunapaswa kutoka kwenye saa sita ama saa saba, kusudi mweze kurudi kwenye shule ya Jumapili asubuhi. Hatutafanya jambo hilo. Sisi... Mkalimani huyu hapa alisema, “Huo si udhuru.” Watu hapo, nami niliona tabasamu dogo likitokea usoni mwa mtu huyo. La. Tutaharakisha moja kwa moja sasa, kwa maneno machache tu ya kutafakari juu ya Neno. Nami kwa namna fulani ni mhubiri mwenye maneno mengi, nadhani.

²² Na nilipokuja miongoni mwa ndugu zangu wa Kipentekoste, miaka kadhaa iliyopita, nilipokuja tu kwa mara ya kwanza, kanisa la Kibaptisti, nilikuwa nikifikiri nilikuwa mhubiri kwelikweli, mwajua, nilibeba Biblia chini ya mkono wangu. Na siku moja nilikuja miongoni mwa Wapentekoste, na Kasisi Bw. Daugherty, nilikuwa nimeshuka kwenda kumsikiliza akihubiri. Jamani, alikuwa amehubiri mpaka akapoteza pumzi yake, akigonganisha magoti yake, na kuziba pumzi. Ungeweza kumsikia kwenye umbali wa majengo mawili ya mji. Karudi, akihubiri tena. Nilikuwa mwangalifu kwa yale niliyosema, wakati huo, kunihusu mimi.

²³ Ndiyo kwanza nije moja kwa moja, na inabidi kwenda polepole. Mimi ni mtu wa Kusini, kwanza, na kwanza ni mtu wa polepole, na daima hucheleva. Na kwa hiyo nivumilieni tu dakika chache, nami nitaharakisha upesi niwezavyo.

²⁴ Lakini ninatumaini ya kwamba Bwana atatupa kitu fulani kidogo hapa kwenye Neno Lake, kusudi litusaidie sisi sote kumkaribia Yeye.

²⁵ Sasa, hapa katika Malaki, mlango wa 3, na sehemu ya kwanza ya kifungu cha 6, ninataka kuchukua somo.

Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu; . . .

²⁶ Ninataka kuchukua somo dogo, kama ikimpendeza Bwana, linaloitwa, “Mungu asiyebadilika hutenda kazi katika njia

isiyotarajiwa.” *Mungu Asiyebadilika Akitenda Kazi Katika Njia Isiyotarajiwa.*

²⁷ Sasa, tunaishi katika wakati unaobadilika. Kila kitu kinabadilika. Kila kitu tu unachoweza kuangalia na kuona kwa macho yako, kinatoka ardhini, na ni kitu kinachofahamika kimwili, na kinaanza kubadilika.

²⁸ Siku chache zilizopita, wakati nilipokuja Phoenix kwa mara ya kwanza, ni... Ziara yangu ya kwanza ya Phoenix ilikuwa ni miaka thelathini na mitano iliyopita, Septemba hii ijayo. Nami niliishi huko nyikani, kwenye barabara ya 16 na Henshaw. Nami nilishuka nikaenda kule chini, nao... nyumba hiyo haipo tena. Kuna kituo cha mafuta, na mji umejengwa pale. Na pia barabara ilikuwa imebadilishwa kutoka Henshaw ikawa—ikawa Barabara ya Buckeye. Loo, kusingekuwako na njia ya kuipata kamwe, kama usingeulizia. Na hayo yametukia katika muda wa miaka thelathini na mitano. Kila kitu ni tofauti sana.

²⁹ Ninakumbuka nikienda ambako ule mradi wa Bonde la Mto wa Chumvi ulipo... mimi na jamaa mdogo tumepanda farasi, tukiwafukuza punda wadogo. Sasa, pana bustani sehemu hizo. Kwa hiyo Phoenix imekua kutoka mlima mmoja hadi mwingine. Imejaza nchi, na ni ninii... Imekuwa na mabadiliko makubwa sana. Usingejua wapi ni wapi. Nilipofika hapa, nafikiri, idadi ya watu ilikuwa yapata watu elfu thelathini na watano ama elfu arobaini. Leo hii ni nusu milioni. Jinsi ambavyo mahali hapa pamebadilika, inaonyesha panaendana na nyakati. Panabadilika jinsi wakati unavyobadilika. Phoenix hubadilika. Mahali pengine hubadilika.

³⁰ Halafu tunajua pia ya kwamba barabara, ninaona, hizo zilibadilika. Barabara mtu ulizokuwa unaingilia huku, haziingii. Haziko tena. Zinaelekea kwingine. Unajaribu kufuatilia alama ulizoingilia wakati mmoja, unapotea, unaishia huko nje nyikani mahali fulani. Kwa hiyo barabara zimebadilika. Miji inabadilika. Na siasa zimebadilika. Zinaendelea kubadilika, mwaka baada ya mwaka. Siasa zinabadilika. Na mataifa yanabadilika. Mataifa, mwaka baada ya mwaka, yanabadilika. Wanabadilisha msimamo wao. Wanabadilisha mipango yao.

³¹ Na ninaona mandhari hubadilika, kama vile miji. Wanakata miti. Wanaishusha milima.

³² Na wao kule Florida, wanatoka nje... Ukishuka na utembe kuambaa ufuko, na, mara ya kwanza unaposhuka kwenda kule, hakuna kitu, maji tu ya pwani. Wakati mwingine, tayari wamejenga kisiwa huko nje mahali fulani, na wamejenga makazi makubwa mapya humo. Wakijitengenezea visiwa, wakiweka pampu kubwa kule chini baharini na kuyavuta maji na kuyapulizia juu, kisha wanakisawazisha kwa mabuldoza na kadhalika, na kujenga mji juu yake, pamoja na nyumba ya kuishi, wakitengeneza visiwa.

³³ Wakilipua vilele vya milima huku nje, ambako, inaonekana, sungura angefika huko kwa shida. Nao wana—wana nyumba huko juu, yenye thamani ya dola laki nyingi. Mandhari yanabadilika.

³⁴ Nasi tunaona, watu wanabadilika. Imefikia ambapo watu siku hizi si wema kama walivyozoea kuwa. Sijui kama mmeona jambo hilo huku ama hamjaona, bali hakika tumeona jambo hilo huko Kusini na Mashariki. Watu wanabadilika, mwaka baada ya mwaka. Wana haraka sana. Inawabidi tu kuharakisha na kutimiza jambo *hili*. Kisha wanatimua mbio barabarani, maili tisini kwa saa, msongamano mkubwa wa magari, kisha wanasimama kwenye baa na kunywa pombe, saa kadhaa, kabla ya kwenda nyumbani. Ni kubadilika, kuharakisha. Wanaenda wapi?

³⁵ Unaona, wanawake wengi siku hizi wana mashine za kufulia, na pasi za umeme, na mashine ya kubonyeza kitufe kuoshea vyombo, na kila kitu jinsi hiyo; nao hata hivyo wana muda mfupi zaidi wa kuomba kuliko walivyopata kuwa nao.

³⁶ Unajua, Susanna Wesley alikuwa na watoto kumi na saba. Naye, akiwa na hao watoto kumi na saba, akichota maji kutoka kwenye chemchemi, na huku anafua kwa mikono yake. Na hata hivyo angeweza kupata saa mbili ama tatu, kwa siku, kuomba pamoja na watoto wake, pamoja na watoto wadogo kumi na saba. Na kutoka humo akatokea John na Charles.

³⁷ Hiyo ndiyo shida ya siku hizi, sababu ya shule zetu kuharibika, hakuna wahudumu wanaoingia, vijana wanaume walio na shauku yake. Tunahitaji wengi zaidi, baba na mama wanaoomba ndio tunaohitaji, kuzifanya shule zetu zijae. Mioyo ya vijana wanaume ikiwaka kwa juhudi kuichukua Injili ndilo tunalohitaji. Lakini mambo yanabadilika.

³⁸ Tungeweza kuendelea mbele kidogo, kwa watu, na kuliingiza kanisani. Kanisa linabadilika. Tunaona hilo, ya kwamba makanisa yetu yanabadilika. Sisi takriban, kweli, tuko hivyo. Ninazungumza kwa kila mahali sasa. Ya kwamba, tuko zaidi sana, inaonekana, tunavutiwa zaidi na kupata idadi kuliko kuwafanya watu waokoke. Inaonekana tu kana kwamba kila mtu anataka kupata idadi kubwa zaidi, ama kuwa na kanisa kubwa kuliko mengine yote, ama jengo kubwa kuliko mengine yote, ama kufanya dhehebu kubwa kuliko madhehebu yote, ama—ama chochote kile, badala ya kufikiria juu ya maskini nafsi iliyopotea. Hilo ni jambo baya sana, bali wapo wengi wetu wanaofanya jambo hilo.

³⁹ Nilimsikia mwinjilisti anayejulikana sana, Ndugu Billy Graham, wakati alipokuwa Louisville, Kentucky. Nilialikwa, na Dk. Mordecai Hamm, rafiki yangu msiri, ambaye Billy aliokoka chini ya mahubiri yake. Nami nilialikwa kuketi kwenye kiamshakinywa pamoja nao. Na Bw. Graham, katika

hotuba yake ya kuvutia, alisema, “Ninaenda kwenye mji, nami nitakuwa...nikae kule majuma sita.” Kasema, “Nitapata labda watu elfu ishirini ambao wata—watakaotubu.” Kisha akasema, “Nitachukua tikiti zao zote, na kadhalika, na kuwapa wahudumu.” Halafu akasema, “Ndipo mwaka mwingine ninarudi,” kasema, “nitazunguka. Na mahali nilipowapata waongofu elfu ishirini, wakati nilipokuwa huko mwaka huo, mwaka unaofuata siwezi kupata hata ishirini.” Kasema, “Kuna shida gani?” Naye...

⁴⁰ Ningetofautiana tu kidogo. Si kutofautiana na mwinjilisti huyo mashuhuri, Bw. Graham, la hasha. Lakini jinsi alivyoliendea hilo, kwa kusema, “Kuna shida gani?” Naye akaelekeza kidole chake, kasema, “Wahubiri wengi kupita kiasi walio wavivu,” akasema, “mnaketi huku mkiweka miguu yenu juu ya dawati, usiku na mchana, wala hamchukui kadi hizi na kuwafuatilia.”

⁴¹ Akasema, “Wakati Paulo alipokuwa hapa, aliingia kwenye mji naye akampata mwongofu mmoja; kisha akarudi tena mwaka uliofuata, alikuwa na thelathini ama arobaini kutoka kwa huyo mmoja. Yeye alikuwa na wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wa wajukuu, wa wajukuu wake, unaona.” Na akasema, “Nina elfu thelathini, nami ninarudi; ama elfu ishirini, ninarudi wala siwezi kupata ishirini.”

⁴² Vema, huenda ikawa ni kwa sababu mimi ni Mpentekoste. Na, bali nilitaka kusema jambo hili sana hata ilikuwa ni vigumu kwangu kutulia. Lakini niliwazia, “Ni mhubiri gani mvivu aliyeveka miguu yake juu ya benchi wakati Paulo alipomfanya aoko?” Unaona? Ilikuwa ni huyo mwongofu, mwenyewe, ndiye aliyeongozwa kwenye kilindi cha Mungu vya kutosha hata akatia nanga.

⁴³ Na kama mtu akitia nanga kwa Mungu kweli, Mungu huingia ndani ya moyo wa mtu huyo. Usiwe na wasiwasi, cheche zitakuwa zikiruka kutoka kila upande, kwa kuwa yeye ameingia kwenye kilindi cha Mungu vya kutosha, na uhai wake wote una shina na msingi katika Kristo, unaona. Kwa hiyo, tunajua ya kwamba si wahubiri wavivu tu. Ni kwa sababu hu—huyo mwongofu haingii ndani vya kutosha mpaka hauoni ulimwengu na mambo ya ulimwengu. Kama akipata kuwa karibu vya kutosha na Mungu, yeye hafanyi hivyo.

⁴⁴ Lakini tunaona ya kwamba makanisa hubadilika na watu hubadilika. Barabara hubadilika. Mandhari hubadilika. Siasa hubadilika.

⁴⁵ Bali kuna jambo moja lisilobadilika, hilo ni Mungu. Yeye anadumu yeye yule. “Mimi ni Mungu, sina kigeugeu.” Haidhuru inachukua muda gani, Mungu kamwe hajabadilika hata kidogo, wala hawezi kubadilika. Ni mahali pa jinsi gani! Sababu ya Yeye

kutobadilika ni kwa sababu Mungu hana kikomo, na chochote kisicho na kikomo hakiwezi kubadilika.

⁴⁶ Na basi hebu na tusome jambo hili kwa muda kidogo kabla hatujayaendea Maandiko. Pasipo na kikomo ni pasipo na kikomo, hakuna—hakuna mwanzo wala mwisho. Yeye—Yeye ni mwenyezi, mwenye nguvu zote, aliyepo kila mahali, anayejua yote; anajua mambo yote, mahali pote, nyakati zote, yuna nguvu zote. Yeye ni Mungu, wala hana kigeugeu.

⁴⁷ Sasa, ninaweza kufanya uamuzi, na kusema itakuwa *hivi*. Nami nina kikomo. Itanibidi kubadilika, kwa sababu mambo huja ambayo, mimi, itanibidi kusema, “Vema, nilikuwa nimekosea.”

⁴⁸ Lakini Mungu hawezi kufanya jambo hilo, kwa sababu uamuzi Wake mmoja ndivyo ulivyo milele. Hawezi kubadilisha maamuzi Yake. Hawezi kuubadilisha.

⁴⁹ Kwa hiyo, kama msimamo wa Mungu kwa mwenye dhambi mmoja na alitaka kutubu, Adamu na Hawa, naye Mungu akawafanyia njia ya kutubu, na Yeye akamsamehe huyo mwenye dhambi; na mwenye dhambi mwingine anakuja, Mungu hana budi kumfanyia huyo mwenye dhambi jambo lile lile, vinginevyo Yeye alikosea wakati alipomtendea mwenye dhambi wa kwanza.

⁵⁰ Na kama mtu alikuwa mgonjwa, na Mungu akamponya mtu mmoja; na kisha kama mtu mwingine akimjia Mungu, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile, la sivyo alikosea wakati alipomponya wa kwanza, kama akija kwa msingi ule ule.

Ni mahali pa jinsi gani pa kupumzikia basi kwa ajili ya nafsi inayotafuta kimbilio!

⁵¹ Sasa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu.” Sasa, tunashangaa jinsi u—ulimwengu ulivyopata kuwa hapa. Unaona, Ne—Neno la Mungu liliumba ulimwengu. Waebrania 11 inatwambia, ya kwamba, “Ulimwengu ulifanywa kwa vitu visivyo dhahiri.” Unaona? Mungu aliunena ukawa, maana Yeye alikuwa ni Mungu. Yeye alisema tu, “Na iwe,” na ikawa. Kwa hiyo, kama . . .

⁵² Hapo mwanzo kulikuwako Neno, nalo Neno lililonenwa lilikuwa ni Neno liumbalo, na kila Neno linalonenwa haliwezi kughairiwa, kama kosa. Basi, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu,” ambaye ni Kristo.

⁵³ Na sasa Neno la Mungu, lililoandikwa katika Biblia, ni Neno Lake kwetu. Na kila ahadi ina nguvu zile zile za uumbaji nyuma yake, ambazo Neno la Mungu lilikuwa nazo hapo mwanzo, kama tukiliamini kwamba ni Neno la Mungu. Inategemea ni wapi mbegu inakoangukia. Kama ikianguka ardhini, a—ardhi inayoweza kuumba. U—unyevu, ama kurutubishwa, kwenye ahadi ya Mungu, italeta kila ahadi iliyofanywa na Biblia. Ni

kama tu ninii...Mbona, nia sahihi ya moyoni kuhusu ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu itaitimiza, kama utaitazama tu, na kulitunza Neno vizuri tu. Kwa sababu Mungu asiye na kikomo alilinen: Neno la Mungu.

⁵⁴ Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Loo, jinsi tunavyopaswa kupumzika juu ya hiyo ahadi ya Kiungu ya Mwana wa Mungu, Ambaye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Hapo ndipo mahali pa kumpumzikia nafsi.

⁵⁵ Sasa, Yesu alisema, katika Neno. Yesu alisema, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu nitalifanya.” Lakini wakati mwingine, Mungu anapotenda jambo fulani na kufanya jambo fulani ambalo tunaomba, hata hivyo hatuninii...Linakuja kwa njia isiyotarajiwa, na wakati mwingine katika mahali pasipotarajiwa, na kwenye wakati usiotarajiwa. Lakini Mungu atajibu katika njia Yake Mwenyewe, kama tu utaamini hilo. Unaona? Unaona?

⁵⁶ Huna budi kuliadini, kulikubali, halafu usilighairi. Lishikilie. Lishikilie, na kusema, “Hili hapa. Mungu alilinen. Hilo latosha. Kama Mungu alisema hivyo, hilo limekwisha, haidhuru ni muda mrefu jinsi gani.” Huenda hapakuwapo na molekuli moja iliyodhihirika wakati Yeye aliposema, “Na iwe” kwa ulimwengu. Lakini, Yeye, Yeye ni wa Milele. Na baada ya kitambo kidogo, molekuli na atomi zilitokea. Nazo zilitokea, kwa sababu Yeye alisema iwe hivyo.

⁵⁷ Na hii hapa ahadi, pia, tunayoweza kuwazia. Kama Yeye, Yeye aliyesema jambo hilo, ametimiza kila Neno, basi atakuwa na kanisa litakalotokea mbele Zake, bila waa wala kunyanzi. Na itatubidi, ndugu, dada, kuwa na hakika kweli ya kwamba tuko sawa na Mungu, na tena kwa sababu kutakuwako na Kanisa, nasi tunataka kuwa sehemu ya Kanisa hilo.

⁵⁸ Haidhuru hii iwe nini duniani, tunautazamia Mji ambao mwenye Kuujenga na Mwenye Kuubuni ni Mungu. Wala hatuwezi kuthubutu kuupoteza huo. Lolote ufanyalo, usisahau jambo hilo. Haidhuru jirani anafanya nini, yale huyo jamaa mwingine anayofanya, yale mwenzio shuleni anayofanya, ama yale mumeo anayofanya, ama mkeo, ama yeyote yule. Ni jambo la ki—kibinafsi kati yako na Mungu. Huna budi, huna budi tu kuutafuta huo wokovu.

⁵⁹ Huenda baba yako alikuwa ni mtu mashuhuri, mama yako mtu mashuhuri, lakini wewe je? Unaona? Unaona? Ni wewe. Huna budi kuupata, wewe mwenyewe. Vema.

⁶⁰ Sasa, wakati Yesu aliposema, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Sasa, hilo liko waziwazi bila kuficha. “Nitalifanya.” Naye alikuwa...Sasa, lina masharti, “Kama utaamini utakapoomba.”

⁶¹ Sasa, katika Marko 11:22, tunaona kwamba Yesu alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ wala usione shaka, bali uamini kwamba hayo uliyosema yatatukia, yatakuwa yako.” Unaona?

⁶² Sasa, sasa, hakika, usingeweza tu kutoka hapa nje na kusema, “Ewe mlima, shuka.” Inakupasa kuwa na kusudi na nia ya kufanya hivyo, unaona. Na kwamba, inakubidi kutafuta kujua, kwanza, kama ni mapenzi ya Mungu, na halafu kusudi lako na nia yako kwa mapenzi ya Mungu. Na ndipo uuambie, na usimame pale. Utashuka, naam, unaona, kama ukiweka hali ya mambo sawa. Lakini inakubidi kuweka hali ya mambo sawa.

⁶³ Sasa, inakupasa kukumbuka, pia, ya kwamba, Mungu anapojibu, wakati mwingine ni katika njia isiyotarajiwa. Yeye hana kigeugeu, bali hufanya mambo katika njia zisizotarajiwa. Sasa, hebu na tuchukue kisa kimoja ama viwili, kabla hatujaendelea.

⁶⁴ Hebu na tuwazie juu ya Musa. Ninapenda kujifunza juu ya Musa. Yeye alikuwa ni mtu hodari sana, naye alitupa Agano la Kale, kupitia nguvu za Mungu.

⁶⁵ Na mara nyingi wenye kushuku husema, “Sasa, Musa aliandika Hilo, basi tunajua kwamba ni kweli?”

⁶⁶ Vema, unaweza kurudi nyuma na kuthibitisha ya kwamba ni kweli. Na kama Yeye ambaye angeweza kusema yale ambayo yamekwisha kuwa, na, ama yale yatakayokuwa, na yale yaliyokuwa yatukie baada yake, na hayo yalitimia, basi ninaamini ya kwamba hayo yalikuwa sahihi, pia, unaona. Unaona? Ni kama—kama tu vile tunavyoweza kusimama hapa juu ya . . . kanisani, naye Roho Mtakatifu anaweza kurudi nyuma maishani mwako na kukwambia kile kilichotukia, na unajua kama hilo ni kweli au la. Vema, kama unajua, na unajua kuwa hiyo ni kweli, basi hakika ungeweza kuamini yale Yeye anayokwambia yatatukia, yatakuwako, kwa maana *hili* linashuhudia *lile*. Unaona? Na hiyo ni kweli.

⁶⁷ Na kwa hiyo tunaona, kama mashahidi, wa Waebrania 11 na mahali pengi katika Biblia, ya kwamba mashujaa wa imani ni wale waliodumu katika ahadi ya Mungu. Dumu tu pale pale, haidhuru mtu mwingine yeyote anasemaje, naye Mungu atakutunukia hilo katika wakati Wake mwema.

⁶⁸ Sasa, Musa alishuka kwenda Misri, ama alikuwa Misri, hasa. Alizaliwa kule. Mtoto mzuri, wazazi wake waliona kwamba alikuwa hivyo, waliona kwamba alikuwa hivyo. Wala hawakuogopa amri ya mfalme.

⁶⁹ Halafu basi wakati, Musa, alifunzwa na mama yake! Ni mwalimu mzuri jinsi gani, mama yake mwenyewe, na angeweza kumhadithia hadithi hizo. “Musa, wewe ni mwanangu, bali ulizaliwa kwa kusudi fulani. Na Mungu atakutumia siku moja kuwakomboa Israeli.”

⁷⁰ Na baada ya kifo cha—cha mama yake wa thamani, basi nadhani Musa alikuwa mtawala mkuu, ama wa pili kutoka kwa Farao pale, alikuwa ni mrithi wa kiti cha enzi. Ndipo siku moja aliwahurumia ndugu zake.

⁷¹ Na hisi wakati mwingine ya jambo fulani, hata hivyo, hata kama tukihisi, inatubidi kutenda katika njia ya Mungu, tupate kuifanya kazi hiyo vizuri. Hakika.

⁷² Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu ana rehema juu ya wote walio na njaa na wanaoteseke, na—nasi tuna kila namna ya—ya mashirika ya kuwalisha wenye njaa na kadhalika. Ninaamini kwamba hilo ni jambo zuri sana. Lakini hata hivyo kazi yenyewe ni Injili. Hiyo ndiyo kazi yenyewe halisi, ni Injili, kuichukua Injili.

⁷³ Sasa tunaona, ya kwamba, baada ya kujikuta kwamba ameshindwa, katika kazi zake mwenyewe. Maana, yeye alikuwa ni mtu mwenye akili nyingi, mwanajeshi. Naye alikuwa hivyo. Alifikuta ameshindwa. Ndipo aka—akaitoroka kazi hiyo, akatoka akaenda nyikani naye alikuwa huko nje kwa muda wa miaka arobaini. Naye alikuwa na mke, na kadhalika, na watoto wake, ama mtoto wake, hasa, Gershomu.

⁷⁴ Sasa, jambo la ajabu ni kwamba, akiwa na wito wa Mungu maishani mwake, ningewazia Musa asingeweza kamwe kuondokana na huo; kamwe asingeweza.

⁷⁵ Na huenda kukawa na watu hapa usiku wa leo wanaotusikiliza moja kwa moja, kwamba kote katika maisha yako, mahali fulani, ulijisikia kulikuwa na wito maishani mwako, wala kamwe hujautikia. Utakuwa mwenye mashaka mradi tu ungali hai, mpaka utakapoyaitikia maisha hayo.

⁷⁶ Halafu hapana shaka kuna watu hapa usiku wa leo ambao wamekuwa wakimtafuta Roho Mtakatifu kwa miaka mingi. Nawe unasema tu, “Vema, si—sijui. Ninapaswa kumpokea. Mimi. . .” Vema, kamwe hutaninii, kamwe hutaridhika mpaka ufanye hivyo, unaona, kwa sababu ulikusudiwa jambo hilo. Na sasa huna budi kulifanya hilo kuwa ndilo jambo la kwanza maishani mwako. Kama utakula tena, ama utakunywa tena, ama kama utalala tena, ama lolote ufanyalo, huna budi kutafuta kitu Hicho. Hiyo ni kweli. Hilo linapaswa kuwa ndilo jambo la kwanza. Jambo ndilo hilo. Dumu tu moja kwa moja na ahadi ya Mungu. Yeye alikuahidi jambo Hilo, kwa hiyo wewe dumu tu nalo, unaona, naye Mungu atalitimiza.

⁷⁷ Sasa, Naye huenda atalifanya jambo hilo katika wakati usiotarajiwa. Unasema, “Vema, Ndugu Branham, nimekuwa nikifanya kazi kwa bidii leo, nami nimechoka kidogo. Wala sijajisikia nafuu kwa muda wa siku tatu ama nne.” Huenda huo ukawa ndio kabisa wakati wenyewe. Unaona? Hujui hata kidogo wakati litakapotukia.

⁷⁸ Ni mara ngapi ningeweza kusimama, na kwa siku kadhaa nisimulie matukio, ninapokwenda mwituni, kumtafuta Bwana, ambapo mi—miiba hunikwaruza, na ndege wananiudhi, na mbu wananiuma. Huo ndio wakati wenyewe hasa ambapo Mungu anajiandaa kufanya jambo fulani, papo hapo. Wakati hasa—wakati hasa jambo fulani linaloonekana halitarajiwi kabisa, ndipo Mungu hujitokeza, kushikilia.

⁷⁹ Sasa mwangalie Musa. Musa, huyu mchungaji wa kondoo mzee mashuhuri sasa, alikuwa tayari ana umri wa miaka themanini. Alikuwa na umri wa miaka arobaini kabla hajachukua msimamo wake kwa ajili ya Mungu. Kisha akachunga kondoo huko mbali, nami naona alikuwa nyikani kwa miaka arobaini. Naye alikuwa anazeeka, labda masharubu yenye mvi, na nywele ndefu zenye mvi zinazoning'inia. Basi alikuwa ndiye huyu hapa, si kanisani; yeye alikuwa chini ya Mlima Horebu. Wala Mungu hakushuka kwa kupitia mahubiri ya injili, bali katika kijiti kilichowaka moto; unaona, wakati usiotarajiwa, mahali pasipotarajiwa, na katika njia isiyotarajiwa.

⁸⁰ Loo, alidhani Mungu angekutana naye huko mahali fulani akiwa na fimbo yake mkononi mwake, ama upanga, ama chochote alichotumia kumwua yule Mmisri.

⁸¹ Lakini Mungu alikutana naye si hata kanisani; chini ya mlima. Mungu alikutana naye si katika nyimbo za dini, bali katika kijiti kilichowaka moto. Wala si alipokuwa kijana, bali alipokuwa mzee. Mungu alimwita akiisha timiza umri wa miaka themanini.

⁸² Wazia jambo hilo. Kwa hiyo wakati mwingine tunafikiri, kwa sababu tuna umri wa miaka thelathini na mitano ama arobaini, vyovyote ulivyo! Wewe kamwe si mzee mno. Una nafsi ambayo haina budi kuishi milele. Kwa hiyo kumbuka tu, ndivyo ilivyo daima: Mungu, Mungu asiyebadilika, katika wakati usiotarajiwa, na katika njia isiyotarajiwa, katika mahali pasipotarajiwa.

⁸³ Hebu na tumchukue Yakobo. Yakobo alikuwa anakimbia. Alishikwa kati ya mioto miwili. Sasa yeye alikuwa akienda nyumbani. Naye Labani, baba mkwe wake, alikuwa anakuja *huku*, akimsaka, kwa sababu mke wake alikuwa ameiba miungu yao. Na tena anakuta kwamba Esau anakuja *huku*, akimfuatilia; ndugu yake, ambaye alikuwa amemdanganya. Sasa, huo ulikuwa ni wakati usiotarajiwa kabisa kwa Mungu kumtembelea. Lakini alikuwa... Huyu hapa Labani anakuja upande *huu*. Naye huyu hapa Labani akija upande *huu*, na Esau upande *huu*. Lakini Yakobo alivuka kile kijito kidogo, na ndipo akaanza kushughulika. Na labda kwa mara ya kwanza maishani mwake, alishika kitu fulani kilichokuwa ni halisi, naye aliweza kushikilia mpaka baraka zilipokuja.

⁸⁴ Hilo lingekuwa ni somo kubwa kwetu sisi sote. Mara ukishika kitu ambacho ni halisi, kishikilie. Usikiachilie. Haidhuru jua linapita juu mara ngapi, ama lolote linalotukia, ni maumivu mangapi ya njaa yanayokuja, chochote cha zaidi, kishikilie mpaka utakapobarikiwa kwacho, mpaka utakapopata ahadi ya kitu hicho. Shikilia.

⁸⁵ Yeye alimweka mkewe, na mambo yote, mbali naye, kisha akajitenga, ndipo akashikilia kwa sababu alizingirwa kati ya mioto miwili. Na Mungu akakutana naye katika njia isiyotarajiwa, katika wakati usiotarajiwa, katika mahali pasipotarajiwa. Hapo ndipo Mungu alipokutana naye.

⁸⁶ Isaya nabii, kijana mwanamume, alikuwa ameegemea juu ya mkono wa mfalme mzuri, naye alikuwa mtu mzuri. Na alikuwa akiishi maisha ya raha. Lakini siku moja huyo mfalme alikufa. Ndipo nabii Isaya akashuka akaenda madhabahuni katika nyumba ya Mungu. Na wakati alipokuwa akiomba pale, alinaswa kati ya dhambi zake mwenyewe na hilo ono. Ndipo akalika kwa sauti kuu, "Ole wangu," wakati alipowaona Malaika waliofunika nyuso Zao kwa mabawa, mabawa juu ya miguu yao, na wakiruka, wakisema kwa sauti kuu, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana." Yeye akapaliza sauti, "Ole wangu, kwa maana mimi ni mtu mwenye midomo michafu." Yeye alishikwa katika wakati usiotarajiwa, mahali pasipotarajiwa.

⁸⁷ Aliwazia, "Nitashuka niende na kusema sala zangu, na kusimama na kwenda, kwa sababu watu wanaamini mimi ni mhubiri mzuri, ama mchungaji, ama kitu kama hicho." Lakini alishikwa pale. Si kwamba tu alishikwa katika hali hii kwa ono, bali alishikwa akiwa na midomo michafu katika nyumba ya Mungu aliye hai.

⁸⁸ Loo, ndugu, kama hilo lingechunguzwa kote katika mji huu usiku wa leo, na kesho asubuhi, kuhusu wahudumu ambao wangesimama na kukwambia ya kwamba hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, wala hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, kungekuwako na wengine zaidi wakipaliza sauti "Ole wangu, niliye na midomo michafu." Ni kweli, naam, ni kweli kabisa.

⁸⁹ Watoto wa Kiebrania, sasa, walishikwa katika hali ngumu pia. Walishikwa katika mahali pasipotarajiwa, ambapo walikutana na Mungu, kusudi Mungu aje kwao kwenye tanuru iliyowaka moto; wakati usiotarajiwa, njia isiyotarajiwa. Lakini Mungu ni asiyebadilika, Mungu asiyebadilika, Naye hufanya mambo hivyo; katika mahali pasipotarajiwa, wakati usiotarajiwa, na kadhalika.

⁹⁰ Israeli waliomba mfalme mwenye nguvu. Walitaka mfalme wa kuwakomboa. Huyo ndiye waliyetarajia Mungu awapelekee, ilikuwa ni mfalme, kuwakomboa, mfalme mwenye nguvu ambaye angetembea mwendo wa kiaskari kama Daudi. "Mwana

wa Daudi angeinuka, ashuke kutoka kwenye ushoroba wa Mbinguni, ashuke atembea duniani katika gwaride kamili la mizinga ya salamu la Malaika, na Baba angeangalia kutoka Mbinguni na kusema, ‘Ninawatumia sasa Masihi.’” Nao walikuwa wameyaandaa yote ya kwamba hivyo ndivyo alivyopaswa kuja.

⁹¹ Lakini walipata nini? Walimpata mtoto mchanga badala ya mfalme mwenye nguvu, mtoto mchanga aliyezaliwa katika zizi do—dogo, ubavuni mwa kilima, zizi dogo la pangoni lenye nyasi kavu, na samadi kutoka kwa wanyama, na m—mtoto mchanga. Lakini lilikuwa ni jibu la maombi yao. Yeye alikuwa kile walichohitaji hasa. Bali walilitaka kwa njia yao wenyewe. Walilitaka jinsi wa—walivyodhani ni bora kabisa. Bali Mungu anajua jinsi ya kulituma jinsi anavyojua ni bora kabisa, kwa maana Yeye ni Mungu asiye na kikomo, Naye anajua tu jinsi ya kulituma.

⁹² Yeye anajua haja zenu. Yeye anajua jinsi ya kuzileta kwenu. Lakini shida ni kwamba, kwa kuwa jambo haliji jinsi mnavyofikiri linapaswa kuja, basi mnakufa moyo kabisa, nanyi mnalirudisha Kwake. Hebu na tumwombe, na tuamini ya kwamba Yeye alalituma jinsi tu anavyotaka kulituma. Na tulikubali juu ya msingi huo. Hiyo ni kweli. Unaona?

⁹³ Kama ukimwomba, usimfanye Yeye kuwa mwongo. Yeye hawezi kusema uongo. Aliahidi, “Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Sasa, Mungu hawezi kusema uongo. Mwombe na litatimizwa. “Tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa.” Tunaamini hilo. Hakika tunaamini.

⁹⁴ Walipata hori. Kwa hiyo walifanya nini? Walimweka Mtoto huyu mchanga horini. Je! huyo alikuwa ndiye Mfalme mwenye nguvu? Walimkataa. Naam, bwana. Kwa nini? Yeye hakuja jinsi walivyomtarajia kuja.

⁹⁵ Na, marafiki, mnaweza mkafikiri hilo lilikuwa ni jambo baya sana. Lilikuwa baya sana. Lakini, mwajua, sisi tuna hatia ya jambo lile lile. Tuna hatia ya jambo lile lile. Tunamwomba Mungu atupe vitu, kisha tunatembea huku na huko, na—na, kama Yeye hamwagi tu kitu fulani juu yetu na kutupa sisi kitu ambacho tunafikiri tunapaswa kuwa nacho, basi tunakirudisha tu. Unaona? Usifanye hivyo. Mwombeni. Kishikilieni moja kwa moja. Naam, bwana. Shikilia hilo kama unajua ya kwamba ni halisi.

⁹⁶ Na ni kitu gani kilicho halisi kuliko Neno la Mungu? “Na Neno la Mungu limefanyika mwili, na likakaa kwetu, Kristo.” Na sasa Kristo alituma Roho Mtakatifu. Naye ni Mungu, katika Roho, kwa hiyo basi shikilia jambo Hilo. Kama Roho Mtakatifu yupo hapa naye ametupa ahadi hiyo, ishikilieni.

⁹⁷ Tuna shida gani sisi, Wapentekoste, ambao tunakiri kwamba tuna Roho Mtakatifu na tunahofu kumtumainia Mungu karibu

kila mahali? Kuna shida gani? Tunatarajia jambo hilo kwa njia fulani nyingine.

⁹⁸ Nafikiri kwamba, kile tunachofanya, nitawaambia kweli, nafikiri tunatarajia jambo hilo, Mungu aingie na kutustawisha huko nje katika dhehebu kubwa mno la namna *hii* na la namna *ile*. Na mkifanya hivyo, mnakuwa na kinyongo dhidi ya jamaa huyo mwingine. Jambo tunalopaswa kufanya, ndugu, ni kusahau kuhusu jambo hilo. Madhehebu yenu ni sawa.

⁹⁹ Bali tunachohitaji ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili wakiwa na wokovu moyoni mwao, na nguvu za Roho Mtakatifu mle ndani, kupendana wao kwa wao, na kunyosha; na kuhurumiana, huruma tukufu, huruma ya matumaini, na upendano wa ndugu. Hayo hutuunganisha pamoja. Hicho ndicho Mungu anachotaka tuwe nacho. Yeye ni Mungu asiye na kikomo, wala Yeye hawezi kubadilika. Maneno Yake, Yeye hawezi kuyabadilisha.

¹⁰⁰ Sasa angalia. Kwa hiyo walimkataa kwa sababu hakuja jinsi Yeye... walivyotarajia liwe. Na tunaona, bali Yeye alikuja katika jinsi ya Kimaandiko. Alikuwa kulingana na m—mpango wa Maandiko hasa. Na kila mmoja wa hawa alikuja, pia, mahali panapofaa, wakati unaofaa, na katika njia inayofaa. Mungu daima hutenda jambo hilo kwa njia Yake, na ndiyo njia inayofaa.

¹⁰¹ Sasa, Musa, kwa nini angetilia shaka? Yeye aliitwa alipozaliwa. Alikuwa mtoto mchanga hapo Mungu alipomwita. Alizaliwa humu ulimwenguni kwa kusudi fulani. Alizaliwa nabii. Lisingekuwa ni jambo gumu kwa Musa kuwazia hilo, kuwa lisilotarajiwa, kwa maana anapaswa kuwa akimtarajia Mungu kumwita.

¹⁰² Yakobo, Mungu alikuwa ndiyo kwanza aseme naye na kusema, “Yakobo, rudi nyumbani. Nitakuwa pamoja nawe na kukuzidisha. Nitaufanya uzao wako kama mchanga wa bahari.” Kwa nini yeye ha—hakutarajia, basi, kwa Mungu kumjia usiku huo wakati Labani alipokuwa akija kwa njia moja, na Esau nyingine? Hata hivyo Mungu alimwahidi. Amina.

¹⁰³ Haya basi, enyi marafiki. Mungu anapotoa ahadi, na upinzani unainuka, hiyo ni kujaribu tu kama kweli umepata Neno, ama hujalipata. Mtu aliye na dhahabu nzuri hajali kwenda kwenye jiwe la kupimia. Unaona? Hiyo ni kweli. Unaona? Ni ninii tu... Petro alisema, ninaamini ilikuwa ndivyo, ya kwamba, “Majaribu haya yamekuja kutujaribu, kutupima,” kuona yale tutakayofanya nayo. Hiyo ni kweli. Unapompokea Roho Mtakatifu, na—na mumeo anaenda kukufukuza nyumbani, ama—ama mama anaenda kukufanya uondoke nyumbani, mambo hayo, usikate tamaa na kurudi ulimwenguni. Huo ni wakati tu wa majaribio.

¹⁰⁴ Yakobo, alipaswa kujua vema zaidi ya jambo hilo. Lakini kwa namna fulani alikuwa ameyatumia vibaya maisha yake, na

kuzurura, na kadhalika, kutoka *hapa, pale*. Naye . . . Ninapenda yale aliyosema pale. “Nilivuka Yordani hii na fimbo tu. Na sasa ninarudi katika majeshi mawili, ninarudi, nimeongezeka sana.” Kisha akasema, “Huyu hapa Esau, ndugu yangu, akija *huku*. Na baba mkwe wangu yuko *hapa*, ananifuatilia.” Na kwa hiyo, wakati alipoingia katika hali kama hiyo, lakini alienda mahali palipofaa, na kuanza kwa kutotarajia, nadhani, kupata jawabu.

¹⁰⁵ Lakini Mungu alishuka, naye akawa na mashindano ya kupigana mwereka, na akakaa pamoja na Mungu, na akashikilia mpaka baraka ilipokuja. Ninampenda Yakobo kwa namna hii. Wakati kweli alipoona jambo fulani lililokuwa ni halisi, wakati alipotia mkono wake kwenye kitu kilicho kweli, yeye alikishikilia mpaka akapata matokeo yake.

¹⁰⁶ Loo, laiti tungalifanya hivyo! Laiti kanisa lingalifanya hivyo tu, laiti mtu ungalishawishika tu ya kwamba ni kweli, na kujua ni ahadi ya Mungu, wala haiwezi kushindwa! Unaninii tu . . . Haiwezi kushindwa.

¹⁰⁷ Mtu fulani akushawishi uiache, aseme, “Ni kwa ajili ya kizazi kingine. Haikuwa kwa ajili yetu.” Na hayo—hayo si Maandiko.

¹⁰⁸ Yesu alisema, katika Marko 16, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” Unaona? Wapi? Umbali gani? Ulimwenguni kote, kila kiumbe. Ishara hizi zitafuata ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe kinachoamini.

¹⁰⁹ Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wale watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

¹¹⁰ Utafanyaje jambo hilo? Injili haina budi kuhubiriwa, na kote ulimwenguni, kuanzia Yerusalemu. Luka 24:49, Yeye alisema, “Kaeni humu mjini Yerusalemu hata mtakapovikwa uwezo utokao Juu.”

¹¹¹ “Baada ya Roho Mtakatifu,” Matendo 1:18, “Roho Mtakatifu akiisha kuja juu yenu, ndipo mtakapokuwa mashahidi Wangu katika Yuda, Samaria, na pande za mbali za nchi.” Kila mahali, Roho Mtakatifu akishuhudia kwa ishara na maajabu yanayofuata.

¹¹² Tutaliachaje jambo hilo? Ni ahadi ya Mungu. Usimruhusu ibilisi. Yeye ni mjanja awezavyo kuwa, na mtu ambaye, inavyoonekana, amesoma Maandiko sana. Bali yeye huwapotosha kuyafanya yaseme ambalo hayasemi.

¹¹³ Na hata hivyo, Biblia ilisema, “Ni dhahiri sana hata mpumbavu asingepaswa kupotea njiani.” Chukua tu ahadi ya Mungu na uishikilie. Shikilia hiyo mpaka utakaposhika

nyingine. Unapoona *hii* ikijibiwa, basi shika *hii*. Halafu shikilia *hiyo* mpaka utakapopata nyingine. Basi endelea tu kupanda.

¹¹⁴ Kama vile kwaya ile ilivyokuwa ikiimba jana usiku, kule kwenye kanisa lile li—lingine, kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, ikisema: raundi ya kwanza ilikuwa ni kuzaliwa mara ya pili, na halafu akaendelea, mwingine akafika mahali pengine. Na punde si punde akapita Mirihi, Jupita, kisha akafika kwenye Kilimia, na akaendelea tu kwenda. Ni—ninapenda jambo hilo. Mnaona? Endeleeni tu kupanda, raundi kwa raundi.

¹¹⁵ Shikilia ahadi ya Mungu, useme, “Mungu, Wewe uliahidi kuniokoa.” Ishikilie. Kaa hapo hapo mpaka utakapookolewa. “Mungu, Wewe uliahidi kunijaza kwa Roho Mtakatifu.” Kaa papo hapo mpaka utakapojazwa na Roho Mtakatifu. Kama wewe ni mgonjwa, sema, “Uliahidi kuniponya. Ninakaa papa hapa mpaka utakaponiponya.” Jambo ndilo hilo. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Kaa nalo.

¹¹⁶ Mungu hana kikomo. Yeye habadiliki. Hawezi kubadilika. Naye anafanya jambo hilo katika njia zisizotarajiwa, bali shikilia mpaka litakapokuja. Usimwambie Mungu nini, jinsi unavyotaka Yeye alifanye. Atalifanya jinsi anavyotaka kulifanya. Unaona? Usimwambie jinsi ya kulifanya.

¹¹⁷ Sasa angalia. Sasa tunaona ya kwamba Isaya alizaliwa nabii. Sasa, yeye alikuwa kwenye wajibu wake wakati alipokuwa kule chini madhabahuni. Halikuwa ni jambo la kigeni kwa nabii kuona ono, kwa hiyo anapaswa kukumbuka. Yeye alikuwa moja kwa moja kwenye wajibu wake. Kwa hiyo, hakuwa nje ya Maandiko; alikuwa moja kwa moja kwenye Maandiko.

¹¹⁸ Mungu alisema, “Kukiwako na mtu miongoni mwenu, ambaye ni wa kiroho, nabii, Mimi Bwana Mungu nitajitambulisha kwake. Yale nabii huyu asemayo yakitimia, basi msikieni. Yasipotimia, mkataeni.” Kwa hiyo, unaona, Yakobo alikuwa anachukuana na Maandiko. Musa, aliendana na Maandiko.

¹¹⁹ Na, Eliya, hebu tumchukue Eliya hapa. Ningetaka kumwambia, sasa, yeye alitoka akaenda huko mbali nyikani na akakaa mwenye huzuni. Ndipo Mungu akamtuma, akamlisha kwa Malaika, na kumweka nyikani, naye akazurura kwa muda wa siku arobaini usiku na mchana. Na muda si muda wajua, ni jambo gani lililotukia? Yeye alikuja, akarudi pangoni. Naye huyo nabii akiwa kule nyuma, alisikia upepo ukienda kasi, ukirushia, ukivuma. Aliisikia miamba ikinguruma, kila kitu. Akawazia, “Vema, hilo ni sawa. Nimekuwa huko juu ya Mlima Karmeli. Ninajua Yeye hujibu, ile ngurumo, na umeme, na mvua. Ninajua jambo hilo.” Lakini, kilichomshika huyo nabii, kilikuwa ni ile Sauti ndogo tulivu isiyotarajiwa.

¹²⁰ Hapo ndipo linapotufanya wengi wetu sisi Wapentekoste turuke. Unaona? Tunatarajia jambo fulani vinginevyo, wakati

Mungu anapolileta kwa njia Yake mwenyewe. Unaona? Tunafikiri ya kwamba, hilo, tunapaswa kuja kwa jinsi tunavyotarajia jambo hilo. Bali Mungu hulituma katika njia Yake Mwenyewe, jinsi anavyotaka kulifanya—kulifanya.

¹²¹ Sasa, Yesu. Wakati walipoomba wapewe mfalme, Isaya 9:6, yeye alisema, “Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto Mwanamume: ufalme Wake utakuwa mabegani Mwake.” “Bikira atachukua mimba, naye atamzaa Mtoto. Ataitwa Imanueli.” Na, loo, Yeye alikuja kulingana na Maandiko hasa. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Jinsi hasa vile Maandiko yalivyosema.

¹²² Musa alikuwa amechukuana, bali halikutokea jinsi alivyodhani lingetokea. Aliwazia, “Nitashuka niende kule na kumwua yule Mmisri. Ndivyo itakavyokuwa, ndipo wana wote wa Israeli watasema, ‘*Nani?*, yeye, mnaona, yeye ndiye shujaa wetu.’” Lakini halikutokea jinsi hiyo. Bali alikuwa bado angali sawa na Maandiko. Yakobo, hao wengine wote, walikuwa sawa na Maandiko wakati Mungu alipotenda kazi.

¹²³ Na tukitii Neno la Mungu, na kulishikilia! “Nifanyeje, Ndugu Branham, nifanyeje nipate kujiweka sawa na Neno la Mungu?” Lichukue tu moyoni mwako na uliamini. Kila ahadi ni yako. Ni yako. Unaweza kuitwaa. Ni mali yako.

¹²⁴ “Kila ahadi katika Kitabu hiki,” unaimba, “ni yangu. Kila mlango, kila kifungu, kila mstari. Ninatumainia upendo Wake wa Kiungu, kwa maana kila ahadi katika Kitabu hiki ni yangu.” Unaona?

¹²⁵ Haidhuru hiyo ahadi ni nini, ni yako hata hivyo, kwa sababu Mungu alikuwa wewe. “Kila atakaye, na aje anywe katika chemchemi, maji ya Uzima, bure.” Ni yako. Ni mali yako. Ahadi yoyote ni yako, kama una imani ya kuitwalia. Na itatendeka, kama tu utaamini.

¹²⁶ Sasa, lakini wakati Yesu alipokuja, tulikuta kwamba Yeye alizaliwa katika hori, kwa hiyo upesi sana Wayahudi walikataa. Yeye hakuja jinsi alivyodhani, walivyodhani Yeye atakuja, kwa hiyo walimtenga tu kutoka kwenye ushirika wao. Wala hakuwa tena ndani yake. Lakini angalia kile alichofanya. Yeye, wakati Yeye. . . Hilo halikumzuia.

¹²⁷ Wakati Pentekoste ilipozaliwa kwa mara ya kwanza, kanisa lilitengwa, pia. Hilo halikuuzua ujumbe. Unaendelea vivyo hivyo. Yesu hawezi kuzuiwa.

¹²⁸ Ni nani anayeweza kumzuia Mungu? Huwezi kumzuia. La. Usingeweza kumzuia. Ingekuwa ni rahisi zaidi kwako kulikomesha jua. Bali huwezi kumpinga Mungu. Mpango Wake utaendelea.

¹²⁹ Kwa hiyo ilifikia wakati makanisa kule nyuma yalipokuwa yakiombea uamsho. Lilitukia kwa njia isiyotarajiwa. Alichukua

kundi la, mtu mmoja mweusi mwenye chongo huku California, na ba—baadhi ya wazururaji wa mtaani, na vitu kama hivyo, na akawajaza na Roho Mtakatifu. Na kuanzisha moto, ambao, angalia mahali umefika sasa.

¹³⁰ Ndilo kanisa linalokua upesi kuliko yote ulimwenguni. Walikuwa na waongofu wengi zaidi mwaka jana kuliko hayo mengine yote yakiwekwa pamoja. Naam. Hiyo ni kweli. *Mgeni Wetu wa Jumapili*, lile gazeti la Kikatoliki, lilisema hivyo. Waliwaandikisha milioni moja na mia tano elfu.

¹³¹ Ni kitu gani? Neno la Mungu linaendelea mbele zaidi, na zaidi, na zaidi. Watu Wake kamwe hawataangushwa. Wao ni askari, amina, maana Neno la Mungu aliye hai linawaka moyoni mwao. Hiyo ni kweli. Mungu anawatumia fedha mahali mbalimbali, akiwabariki, akiwaleta. Sasa hebu na tuweke nia yetu kwenye Neno, na juu ya Mungu, na tuendeleo kusonga mbele.

¹³² Sasa, msiliondoe, mkisema, “Sisi tutakuwa kundi lililo kubwa kuliko yote. Ama, tuna kundi lililo bora sana mjini. Umati uliovalia nadhifu sana huja kwetu,” ama kitu kama hicho. Ukiweka hicho niani mwako, umeanguka papo hapo. Unaona? Naam, bwana.

¹³³ Kumbuka tu, popote alipo Roho, ndipo palipokuwa na wale wenye Uhai. Hiyo ni kweli. Dumuni na Roho wa Mungu. Lolote mnalofanya, dumuni na Roho huyo.

¹³⁴ Sasa, Yesu, wakati alipokua, Yeye alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi ambaye walikuwa wameomba. Yeye aliwaonyesha ishara Yake ya Masihi. Alithibitisha ya kwamba alikuwa ndiye Masihi, kwa ishara alizofanya.

¹³⁵ Hebu mwangalie yule mwanamke pale kisimani wakati Yeye alipomwambia dhambi zake, ya kwamba alikuwa na waume watano. “Loo,” alisema, “Bwana, tunajua atakapokuja Masihi, atatwambia mambo yote.” Bali hakujuu Yeye alikuwa ni Nani.

Akasema, “Mimi Ndiye.”

¹³⁶ Mwangalie Nathanaeli, wakati aliporudi pamoja na Filipo, naye akaenda Mbele ya Yesu. Naye Yesu akamwambia yeye alikuwa ni nani, mahali alikotoka, yale aliyokuwa akifanya. Loo, jamani! Iithibitisha. Yeye alisema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Jamani! Hakika. Maana, yahuu nini? Alithibitisha. Alikuwa ndiye. Alikuwa ninii... wao...

¹³⁷ Yeye hakuletwa jinsi Israeli walivyodhani ataletwa. Walifikiria, “Yeye atakuwa ni Mfalme mwenye nguvu akiwa na fimbo mkononi Mwake, na atatoka aende akawapige Warumi kichwani nayo.” Bali hiyo haikuwa njia ya Mungu.

¹³⁸ Hilo hata halikuwa ni Maandiko yamhusuyo Yeye kufanya jambo hilo katika kuja huko. Kuja mara nyingine ndipo Yeye

atakapofanya jambo hilo. Wao walichanganya kuja mara ya kwanza na mara ya pili, pamoja.

¹³⁹ Wakati huo Yeye alikuja akiwa mnyenyekevu, mpole, ameketi juu ya nyumbu, amepanda akiingia. Na Yeye alitoka kwenye—kwenye ninii—kwenye mji ulio mdogo kuliko yote wa mikoa yote mi—mikubwa. Na loo, Maandiko yalitimiza tu kuja Kwake, jinsi atakavyokuja, bali walishindwa kuona jambo hilo. Unaona? Lakini Yeye alifanya ishara ya Masihi, akathibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, nao wakaikataa kwa sababu alikuja kwa njia isiyotarajiwa kwao. Sasa, laiti wanalikuwa tu tayari kumkubali juu ya misingi ambayo Mungu alimtuma!

¹⁴⁰ Je! sisi twaweza usiku wa leo, kama Wapentekoste, kumkubali Roho Mtakatifu juu ya misingi ambayo Mungu alimtuma? Je! tunaweza kumtarajia Roho Mtakatifu kufanya yale Mungu alisema Yeye angefanya wakati atakapoingia? Je! huo ndio msingi tunaotaka kumkubalia? Ama tunataka kusema, “Loo, ninaamini nilimpokea Roho Mtakatifu *wakati* nilipoamini. Nilimpa mchungaji wangu mikono, na, nakwambia, ni—ninaamini nina Roho Mtakatifu”? Hivyo siyo Biblia ilivyoosema.

¹⁴¹ “Wakati atakapokuja, atanishuhudia Mimi,” Yesu alisema, unaona, atakapokuja.

¹⁴² Sasa, Yeye anashuhudia juu—juu ya Mungu? Anashuhudia kwa maisha anayoishi ndani yako. “Kwa matunda yao mnajulikana.”

¹⁴³ Ungeweza kusema, “Vema, Ndugu Branham, nilimpata Roho Mtakatifu. Nilinena kwa lugha.”

¹⁴⁴ Ninaamini hilo, pia. Lakini kama maisha hayo hayafuatani na tukio hilo, basi kulikuwa na kasoro fulani, unaona, ulipata kitu kibaya. Unaona? Lakini kama una—kama ulimpata Roho Mtakatifu halisi, na ulinena kwa lugha, basi maisha yanafuatana naye. Halafu basi, kama ukidai una Roho Mtakatifu, nawe ulikuwa na tukio, halafu maisha yako hayalingani na Neno la Mungu, basi una roho mwovu. Unaona? Maana, “Huwezi kuchuma zabibu kutoka katika m—mbaruti.” Unajua jambo hilo. Unaona? “Na kwa matunda yao wanajulikana.”

¹⁴⁵ Naye Yesu, wakati alipokuja, akithibitisha Yeye alikuwa ndiye Masihi, alifanya kazi za Masihi. Amina. Alisema, “Kama sifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini. Lakini kama ninafanya kazi za Baba Yangu, basi aminini kazi hizo.” Ni tamshi la jinsi gani! Ndivyo ilivyo siku hizi, kama Yeye alivyoahidi katika Waebrania 13:8, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹⁴⁶ Madhehebu, madhehebu makubwa ya dunia, yanatarajia nini yanapoona ninii... uamsho ukitokea mjini? Madhehebu yanatarajia nini? “Hotuba kubwa ya kiakili. Inampasa kuja kwa elimu nzuri, maneno mazito. Na aweze, awe na mvuto, wa

kupata ushirikiano kila mahali, na—na kila kitu namna hiyo, na mpango mkubwa mno.” Unafanya nini? Mnaenda madhabahuni, kundi la Mayezebeli waliojipodoa ambao hawajawahi kujiosha, kundi la jamaa wavuta sigara wanaodai kuwa ni Wakristo, wala hawajapata kuyanyosha maisha yao, yangali ni maovu kama pipa la majoka. Ati unaniambia ya kwamba huyo ni Roho Mtakatifu? La, bwana.

¹⁴⁷ Roho Mtakatifu ni utakatifu, na nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo. Biblia ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Amina. Hiyo ni kweli, ndugu yangu, sio kuwadharau. Lakini ninii...

¹⁴⁸ Ni kitu gani? Hebu mpeleke mtu pale juu, huenda akagugumiza maneno kidogo, na kutatarika kidogo katika lugha yake, na kuyaendeleza maneno kadhaa vibaya, ama kuyatamka vibaya. Ndipo wanasema, “Aha, jamaa huyo hana lolote.”

¹⁴⁹ Vipi kuhusu Dwight Moody wenu, mmoja wa watu mashuhuri sana mliopata kuwa nao tangu Charles Finney. Hiyo ni kweli. Vipi kuhusu Moody? Ilikuwa vigumu kwake kulisoma jina lake, maskini mzee mshona viatu.

¹⁵⁰ Siku moja, huko, alikuwa akiwahubiria wakukni huko Uingereza, naye akajaribu kuisoma Biblia na akatamka maneno vibaya. Ati nini? Yeye, nafikiri, aliwaita Wafilisti, “Wafilisti,” ama kitu kama hicho, namna fulani ya neno alilojitungia. Akarudi nyuma nusu ya kifungu hicho. Akajaribu tena. Alifikiri angekuwa na wakati wa kuliendeleza. Akalikosa tena. Akarudi akasoma kitu hicho chote tena, naye akalikosa tena.

¹⁵¹ Akafunga Biblia. Naye alijua ya kwamba hao wakukni walikuwa wameketi pale, kuniniii tu... Halina budi kuwa ni la kielimu kwao. Akaifunga Biblia. Naye akasema, “Bwana Mungu, nitazungumza kwa lugha uliyonituma nayo.” Ndugu, alipararua mahali hapo vipande-vipande. Alipararua. Machozi yalitiririka mashavuni mwake.

¹⁵² Gazeti moja lilikuja kuchunguza, kuona ni namna gani alikuwa akiwavutia watu wengi sana. Basi gazeti hilo lilikuja na kuandika makala moja, likasema, “Ni kwa nini mtu yeyote aje kumwona Dwight Moody?” Akasema, “Jambo la kwanza, yeye ni mshamba sana ukimwanguka.” Kisha likasema, “Jambo la pili,” likasema, “yeye huzungumza kwa pua yake. Hana—hana hotuba nzuri.” Tena likasema, “Sarufi yake ni mbaya kupindukia.” Na likasema, “Ana sura mbaya sana. Yeye ni mnene, mwenye umbo la mviringo, na masharubu kote usoni.” Loo, walimwita kila kitu, karibu kila kitu.

¹⁵³ Meneja wake alikuja na kusema, “Bw. Moody, haya hapa yale gazeti liliyosema kukuhusu wewe.” Akasoma yalivyokuwa. “‘Bwana,’ kasema, ‘kwa nini mtu yeyote aje kumwona Moody?’”

¹⁵⁴ Basi Bw. Moody aliyatupilia mbali kwa sentensi moja, kasema, “Aha. Kweli kabisa. Wao wanakuja kumwona Bwana.”

Hivyo tu. Hawakuja kuninii . . . Kama unakuja kumwona Dwight Moody, hilo ni jambo lingine; inakubidi kuwa kitu cha kuangaliwa.

¹⁵⁵ Ndugu, kama unakuja kwa ajili ya hotuba ya kiakili, hiyo ndiyo unayotafuta, hiyo ndiyo unayotarajia. Lakini kama unakuja kuona nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu, itahitajika nguvu za Mungu kutoka Mbinguni kufanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Inategemea unatafuta nini, kile unachotarajia.

¹⁵⁶ Ninapokuja kanisani, ninatarajia wokovu. Ninatarajia watu watakatifu. Ninatarajia kundi lililosafishwa kutokana na maisha ya dhambi. Hayo ndiyo unayotarajia, maana hayo ndiyo Mungu anayohitaji. Lakini mnaona jinsi tunavyolegeza mambo?

¹⁵⁷ Maskini Ndugu Spurgeon, mhudumu mzee Mmethodisti rafiki yangu, alizoea kuhubiri kuhusu, kasema tulishusha . . . ama kuzungumza, kuimba juu ya, hasa. Alisema:

Tumezembea, tumezembea,
Tumepatana na dhambi;
Tumezembea, kondoo wakatoka,
Lakini mbuzi waliingiaje?

Kuzembea, hiyo ni kweli, kuzembea.

¹⁵⁸ Dumuni na Neno. Mungu hakosei. Mungu ni Yule asiye na Kikomo asiyeweza kubadilika. Yeye habadiliki, Mungu asiyebadilika, Yeye yule aliyeshuka katika Siku ya Pentekoste, na kuijaza nyumba yote kwa upepo wa nguvu ukienda kasi. Na ndimi za Moto zilizogawanyika zikawakalia, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. Huyu ndiye Mungu yeye yule tunayetarajia kumwona leo. Inategemea unatafuta kitu gani. Mungu asiye na kikomo, “Mimi ni Mungu, wala sina kigeugeu.” Yeye habadiliki. Hawezi kubadilika. Kama hicho ndicho alichowapa hao wenye matarajio wa kwanza huko nyuma, hicho ndicho atakachowapa wenye kutarajia wa pili, hicho ndicho atakachowapa wa tatu, wa nne. Na kila mtu atakayemwita litakuwa ni jambo lile lile.

¹⁵⁹ Yeye alisema, “Mimi ni Mzabibu. Ninyi ni matawi.” Kama mzabibu ukitoa tawi, nalo lizae zabibu, mzabibu wa pili ama . . . Tawi lingine ambalo mzabibu huo utachipuza litazaa zabibu. Huwezi kufanya moja lizae boga, lingine, tikitimaji, na halafu zabibu. Huwezi kufanya jambo hilo. Unaona, inaonyesha ya kwamba limetupwa. Ni ninii—ni mzabibu ambao umepandikizwa. Hiyo ni kweli. Ama mzabibu fulani ambao umeninii . . . ama tawi fulani ambalo limepandikizwa katika mzabibu.

¹⁶⁰ Nilikuwa nimesimama hapa wakati mmoja pamoja na Ndugu John Sharritt. Alinionyesha kama, loo, kama matunda manne ama matano ya jamii ya machungwa kwenye ninii . . . kwenye ninii . . . mti. Ninaamini yalikuwa ni makomamanga.

Na—na, la, labda nimekosea hapo. Yalikuwa ni machungwa, na malimau, na machenza, na makangaja, na mabalungi, yote yakikulia kwenye mchungwa.

¹⁶¹ Nikasema, “Lakini, Ndugu John, ninataka kukuuliza jambo fulani. Yatakapochipuza sasa, na kuchipusha matumba tena,” nikasema, “je! yote yatakuwa ni machungwa?”

¹⁶² Akasema, “La. Kila moja la tawi, kila moja la hayo matawi madogo yaliyokatwa na kupandikizwa kwenye mti huu. Kama ni mlimau, utaninii. . . Kama ni tawi la mlimau, litazaa malimau.”

¹⁶³ Nikasema, “Lakini vipi kama mti huo wa asili ukichipuza tawi lingine?” Akasema, “Linazaa machungwa.” Hiyo ni kweli.

¹⁶⁴ Kwa hiyo, ndugu, tunaweza kujirusha ndani kwa dhehebu. Hilo tu ndilo tulilo nalo. Tunazaa matunda ya kimadhehebu. Tunazaa ushuhuda wa kimadhehebu. Lakini kama umezaliwa na ule Mzabibu, nao ukuzae wewe, kiumbe kipya katika Kristo, utazaa maisha ya Kristo. Kwa hiyo nisaide, utayazaa. Kweli. Utakuwa na tukio lile lile walilokuwa nalo hapo mwanzo. Amina. Ninajua ni kweli.

¹⁶⁵ Madhehebu huwatafuta wenye bongo. Shida, sisi Wapentekoste, tunatafuta sana upepo unaoenda kasi, tunaikosa ile Sauti ndogo tulivu. Hivyo tu ndivyo ilivyo. Unaona? Naam, bwana. Halitarajiwi, wakati mwingine. Kama halina Sauti ndogo tulivu ndani yake, vema. . . Ama, inayo mle, vema, hatutaki kulikubali. Mara nyingine mafundisho mazuri kweli, mara nyingine, hutukatakata tu vipande-vipande, kwa namna fulani yanatutumua manyoya yetu kidogo, unajua. Wakati mwingine hilo hutusaidia kidogo. Mnajua hiyo ni kweli. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ni kweli, naam, bwana, jambo fulani litakalotusaidia, kutufanyia mema.

¹⁶⁶ Sasa, Eliya alikuwa amesikia pepo zikienda kasi, naye alijua huyo alikuwa ni Mungu huko nje, ama kitu fulani kikipita. Alisikia mvua, kila kitu. Lakini kilichomshitua ni wakati Yeye alipokuja katika hiyo Sauti ndogo tulivu. Alikuwa amemwona akija katika mvua. Alikuwa amemwona akija katika moto, pia. Alisikia pepo. Na alisikia mvua. Alisikia moto, na akaona huo moto, na kadhalika. Lakini alishtuka wakati hiyo Sauti ndogo tulivu ilipokuja. Kwa hiyo aliweka utaji kwenye uso wake na akatoka nje. Loo, ndugu, jambo ndilo hilo.

¹⁶⁷ Tunachopaswa kufanya ni kusikiliza ndani kabisa kwenye kilindi cha moyo wetu mpaka tuisikie Sauti ya Mungu, kisha tutoke nayo, tuamini ya kwamba ni kweli. Naam, bwana.

¹⁶⁸ Mimi, lakini ninashangaa leo, ndugu, kama tunakosa kutambua, hata hivyo, Roho Mtakatifu miongoni mwetu. Nashangaa kama watu katika mielekeo yetu leo, kama hatushindwi kutambua ya kwamba huyu ni Roho Mtakatifu. Unaona?

¹⁶⁹ Sasa, ninajua, kwa baadhi yenu ninyi wageni, labda, huku kambini usiku wa leo, huenda baadhi ya watu wakaishi maisha ambayo ungeona aibu kuyaishi, wewe mwenyewe. Huenda hilo likawa ni kweli. Lakini, ndugu yangu, dada, hao hawana yale wanayozungumzia. Hilo ni kweli. Hilo ni kweli. Lakini kamwe usiamue kwa jambo hilo.

¹⁷⁰ Nilipokwenda India, kulikuwa na mtu aliyetaka kunithibitishia angeweza kulalia msumari. Mmoja alitaka kutembea motoni. Alitaka kufanya mambo haya yote, kuonyesha yale angeweza kufanya, kwa nikeli moja, ama shilingi, ama peni, chochote ambacho unempa. Lakini, sikilizeni, yeye alikuwa akicheza sehemu ya mnafiki kule nje. Lakini huko nyuma kabisa barani kulikuwako na mtu mwaminifu, alikuwa akifanya hivyo kabisa, wakifikiri walikuwa wakimtolea mungu fulani dhabihu mahali fulani. Lakini alikuwa akicheza sehemu ya mnafiki.

¹⁷¹ Tuna jambo lile lile. Hiyo ni kweli kabisa. Baadhi ya wanaume, wanawake, wananinii tu...ama wanaojiita, wanajaribu tu kuiga, na kufanya kana kwamba wana Roho Mtakatifu, na ni kwa sababu tu hao wengine huenda hivyo.

¹⁷² Kama nilivyokuwa nikisema, hivi majuzi usiku. Wakati nilipoingia mimbarani kwa mara ya kwanza, ni—nilienda pale juu, nami ni—nilimwangelia Dk. Davis jinsi alivyohubiri. Na ndiyo kwanza tu nipate leseni ya mtoa hotuba, kwa hiyo nikaenda pale juu. Nikawazia, “Aisee, mnajua nini? Ninaweza kuhubiri namna hiyo pia.”

¹⁷³ Kwa hiyo nikapanda pale na kurusha mikono yangu jinsi yeye alivyofanya, na *nikarukaruka* jinsi alivyofanya, nami nilikuwa tu nikisema, “Haleluya! Utukufu kwa Mungu!” Na, “Haleluya! Utukufu kwa Mungu!” Na, “Haleluya! Utukufu kwa Mungu!”

¹⁷⁴ Halafu basi, muda si muda wajua, niliposhuka kutoka pale, wanawake wote wazee walikuja wakanizunguka na kusema, “Loo, huo ulikuwa mzuri sana, Billy!”

¹⁷⁵ Lakini maskini mzee Dk. Davis aliketi pale, mwanasheria wa siku nyingi, mwajua, akaniangalia namna *hiyo*. Nikasema, “Nilifanyaje, Dk. Davis?”

¹⁷⁶ Kasema, “Uozo. Mbaya sana niliopata kusikia.” Loo, jamani, kweli alinipunguzia majivuno! Kasema, “Ninakutaka kwenye chumba changu cha kusomea kesho alasiri, saa nane.”

Nikasema, “Vema, Dk. Davis.”

¹⁷⁷ Nikaingia, huku nimeabika sana, mwajua. Akaniangalia, kasema, “Nadhani unajisikia kana kwamba kamwe hutanisamehe, Billy.”

Nikasema, “La, ninataka kujua ni kwa nini.”

¹⁷⁸ Akasema, “Wakati nilipoanza kufanya kazi ya uanasheria,” akasema, “nilimwangelia mwanasheria mmoja. Na hapana

shaka hivyo ndivyo umefanya pia: uliniangalia.” Akasema, “Kwa sababu, nilikuona ukijaribu kupitia kila tendo nililopitia.”

¹⁷⁹ Akasema, “Lakini unajua nini?” Kasema, “Sababu ya mimi kusema ‘uozo kabisa niliopata kusikia,’” akasema, “ni kwa sababu kamwe hukuleta Neno la Mungu hata kidogo. Ulikuwa tu ukilia, na kukoroma, na kutoa udenda na kupiga kelele.” Kasema, “Kamwe hukusema kitu kuhusu Neno,” kasema.

¹⁸⁰ Na kwa hiyo akasema, “Nilipanda nikaenda pale na kujaribu kupita na kutetea kesi ya talaka. Ndipo nikasema, ‘Maskini mwanamke huyu! Boo-hoo! Maskini mwanamke huyu! Boo-hoo!’ Nikaendelea namna hiyo.”

¹⁸¹ Kisha akasema, “Mwanasheria mzee aliketi pale na kuangalia namna *hiyo*, kwa kama nusu saa, mpaka nilipomaliza kupigapiga na kulia, mpaka karibu niishiwe na sauti.” Kasema, “Huyo mwanasheria mzee akasema, ‘Hakimu, Mheshimiwa. Mahakama yako itavumilia upuuzi wa namna hii kwa muda gani zaidi?’”

¹⁸² Akasema, “Nikasema... Nikamwendea maskini mwanasheria huyo wa siku nyingi, naye akaniambia. Akasema, ‘Unajua nini? Ulikuwa ukipiga kelele nyingi na kila kitu. Wewe—wewe ni hivyo, vema. Lakini,’ kasema, ‘hukuwa ukielezea sheria yoyote. Inahitaji sheria kushinda kesi.’”

¹⁸³ Ndugu, hivyo ndivyo ninavyofikiri usiku wa leo pia. Inapaswa kuwa ni jambo lile lile, ndugu. Haidhuru una kiasi gani cha elimu, akili, na chochote kile tulicho nacho, inabidi kuweko na nguvu fulani na dhihirisho la Roho Mtakatifu kuthibitisha ya kwamba ni Mungu, ambaye atayanyosha maisha yako, yatakayotenda na kufanya Maisha yale yale Yesu Kristo aliyofanya. Amina.

¹⁸⁴ Aliahidi katika siku za mwisho ya kwamba Yeye angeninii... “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Nabii aliahidi jambo hilo. Tunaona nuru kijiografia huchomoza mashariki na kutua magharibi. Na jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linalotua magharibi. Tunajua hiyo ni kweli.

¹⁸⁵ Sasa, ustaarabu ulianzia wapi? Mashariki. Hiyo ni kweli. Umesafiri pamoja na jua, na sasa uko kwenye Pwani ya Magharibi. Ukienda mbali zaidi, utarudi mashariki tena. Mashariki na magharibi vimekutana, ustaarabu. Tunataka mwone jambo hili kwa muda kidogo tu.

¹⁸⁶ Sasa, kumbukeni, nabii alisema, “Kutakuwako na siku ambayo haitakuwa nuru wala giza, siku ya utusitusi. Lakini wakati wa jioni, itakuwa Nuru.” Sasa angalia. “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

¹⁸⁷ Sasa, Mwana wa Mungu aliangaza haki Yake na nguvu Zake juu ya watu wa mashariki yapata miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Na kumekuja kipindi cha wakati ambapo tumekuwa

na mafundisho ya kiakili. Tumekuwa na wakati mzuri sana. Tumeunda madhehebu. Tumefanya kazi kuu, ambalo ni sawa. Ni siku tu ya utusitusi.

¹⁸⁸ Sidhani mnayapata hapa Phoenix, bali huko mashariki tunayapata, mawingu-mawingu hivi, nuru ya kutosha kwenda huku na huko; bali jua haliwaki. Linawaka mahali fulani, kwa sababu wewe... Kusingekuwako na nuru kama halikuwa likiwaka. Lakini hasa si nuru nzuri ya jua. Lakini basi wakati wa jioni, mawingu yanarudi nyuma, na jua lile lile lililoangaza mashariki linaangaza magharibi.

¹⁸⁹ Ndipo Yesu yeye yule, Roho Mtakatifu yeye yule aliyewashukia watu wa mashariki, ameshuka katika siku ya madhehebu, na akashuka hapa katika siku za mwisho, kuangaza Nuru juu ya magharibi ya mbali. Ni Yesu yeye yule, jambo lile lile, Yeye yule mwenye upendo.

¹⁹⁰ Yeye yupo hapa usiku wa leo katika umbo la Roho Mtakatifu. Huja! Yeye ni—Yeye ni Mungu asiyebadilika. Yeye kamwe hawezi kubadilishwa. La. Yeye huja katika njia zisizotarajiwa, akitenda maajabu, njia mbalimbali, kutenda maajabu yake. Njia za siri, hasa, kutenda maajabu yake.

¹⁹¹ Lakini kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Hakuna mtu anayeweza kutilia shaka hilo, kadiri alivyosema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Sasa, wakati wa Sodoma, hilo lilikuwa ni kabla tu ya ule moto kushuka na kuuteketeza Sodoma na Gomora. Na sasa tunakaribia tu ile saa ya usiku wa manane, kwa ajili ya Kuja Kwake Kristo mara ya pili, na ulimwengu kuangamizwa kwa moto.

¹⁹² Ni jambo gani lililotukia? Kulikuwako na matabaka matatu ya watu katika siku hiyo, na kuna matabaka matatu ya watu leo. Kwanza, kulikuwako na Wasodoma; ulimwengu. Kulikuwako na Lutu na watu wake; kanisa, la kawaida, jamii ya wasomi. Na kulikuwako na Ibrahimu pamoja na kundi lake; Ibrahimu na kundi lake, wameketi kule juu, Kanisa Lililoteuliwa na lililoitwa litoke.

¹⁹³ Kumbukeni, sasa, kulikuwako na makundi matatu. Wasodoma; wenye dhambi, dunia ya waovu kama ilivyo siku hizi. Kulikuwako na mfuasi wa kanisa, vuguvugu, baridi; Lutu, kundi lake. Kulikuwako na Ibrahimu, aliyeitwa atoke humo, naye alikuwa ameketi huku nje nyikani, akistahimili mambo magumu. Kweli. Na Bwana akashuka katika mfano wa Mwanadamu, Msemaji wa hawa Malaika watatu waliosimama.

¹⁹⁴ Sasa, mtu fulani aliniuliza, kasema, “Ndugu Branham, huamini huyo alikuwa ni Mungu?”

¹⁹⁵ Nikasema, “Alikuwa Mungu. Kwa sababu, sasa, sikilizeni. Ibrahimu alimwita, herufi kubwa B-w-a-n-a. Na msomi yeyote

anajua ya kwamba hiyo herufi kubwa B-w-a-n-a ni Elohimu, ambaye ni Mungu.”

¹⁹⁶ Akasema, “Vema, Yeye kwa vyovyote angewezeje...” Nikasema... Yeye akasema, “Ati Mungu, akila?”

¹⁹⁷ Nikasema, “Hakika.” Nikasema, “Mungu alinyosha tu mkono akachukua konzi ya—ya nurulimwengu, na chochote kile cha ziada kilichombidi kukusanya, na petroli kidogo, na nurulimwengu, na—na kalisi kidogo, na chumvichumvi. Akasema, ‘Whiu! Ingia katika huo, Gabrieli. Whiu! Ingia katika huo, Mikaeli.’ Naye akaingia, Mwenyewe.”

¹⁹⁸ Yeye ni Mungu. Unashindwa kuona kwamba Yeye ni Nani. Yeye ni Mungu asiyebadilika. Nina furaha nina imani ndani Yake usiku wa leo, ya kwamba siku moja wakati maisha yangu, mwili wangu ukiwa na elementi zake kumi na sita utarudi kwenye mavumbi ya ardhi. Lakini Yeye atasema, “William Branham,” nami nitatokea. Yeye ataupulizia pumzi ya uhai, aseme, “Haya basi.” Ataepa kuzaliwa—kuzaliwa kupitia kwa mama yangu, na kadhalika.

¹⁹⁹ Kama vile Yesu, katika mwujiza Wake wa kwanza, Yeye aligeuza maji yakawa divai. Hatimaye yangekuwa ni divai, lakini alivuka utaratibu huo wote, na kusema, “Yageuze maji yawe divai.”

²⁰⁰ Kwenye ule ufufuo, Yeye hatasema, “Bw. na Bi. Branham fungeni ndoa tena mkamzae William.” Atanena, nami nitatokea. Amina. Huyu ni Yeye. Yeye ni Mungu.

²⁰¹ Hakika, alikula. Alishuka akaenda kule mbele ya Ibrahimu. Sasa, angalia yale aliyofanya sasa.

²⁰² Kumbukeni, Wao walikuwa wakishuka kwenda huko, wawili wa wale Malaika walishuka wakaenda na kuhubiri huko Sodoma. Hilo ni kweli? Walifanya mkutano kule chini. Lakini Walifanya nini? Hawakufanya miujiza mingi mno, bali Walifanya nini? Waliwapofusha hao Wasodoma.

²⁰³ Na sasa tuna malaika hao hao wakihubiria kanisa la kawaida siku hizi: akina Billy Graham, na kadhalika. Na ni kitu gani kinachoupofusha ulimwengu? Ni Neno. Na kuhubiri Neno, kunampofusha asiyeamini.

²⁰⁴ Lakini liangalie Kanisa hili Teule, lililoitwa litoke, huyu Malaika aliyenena pale na Ibrahimu.

²⁰⁵ Yeye, sasa kumbukeni, jina lake lilikuwa Abramam mpaka siku chache tu hapo kabla. Na jina la mke wake lilikuwa Sarai, S-a-r-a. Lakini, yeye, Mungu alikuwa amekutana na Ibrahimu katika umbo la Roho, na alikuwa amebadilisha jina lake kutoka Abramam likawa Ibrahimu, kutoka Sarai likawa Sara.

²⁰⁶ Na sasa mwangalie Malaika huyu, mavumbi nguoni Mwake, Naye alisema, “Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sara?”

207 Nashangaa. Hapana budi Ibrahimu alisema, “Uo—uongozi wangu ulikuwa ni wa kweli. Nilisikia tu kitu fulani. Jamaa huyo alikuwa tofauti.”

Akasema—akasema, “Yumo katika hema iliyo hapo nyuma Yako.”

208 Alijuaje alikuwa na mke? Alijuaje jina lake lilikuwa limebadilishwa? Alijuaje hayo, mama huyu, hali hizi? Kasema, “Nitakurudia wakati huu huu mwakani.” Yeye hata alijuaje Ibrahimu alikuwa ameo? Unaona? “Yu wapi mkeo, Sara?”

209 Akasema, sasa angalia, “Mimi,” hicho kiwakilishi nafsi hapo, “Nitakurudia majira kama haya mwakani.” Mnaona huyo alikuwa ni nani. Mnaona? Mnaona Yeye alikuwa ni nani. Na Yeye—Yeye akasema. . .

210 Na Sara, hemani, akasema, “Ninawezaje?” Akachekeka. Kwa maneno mengine, kuchekeka kifichifichi, mwajua, kimoyomoyo, akasema, “Sasa angalia. Ninawezaje kupata raha tena?”

211 Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, nayo Biblia inasema dhahiri hapo sasa, ya kwamba wote wawili walikuwa na umri mkubwa, na ni wakongwe. Naye Sara alikuwa amekoma katika desturi yake kwa muda mrefu. Ibrahimu, mwili wake ulikuwa kama umekwisha kufa. Naye mke tumbo lake la uzazi lilikuwa limekauka na limekufa, kwa muda wa miaka kadhaa.

212 “Nitakurudia majira kama haya mwakani, majira kama haya mwakani, nawe utamzaa mtoto huyu.”

213 Sasa angalia, kabla ya kufunga. Naye Sara akachekeka, akasema, “Jambo hilo kwa vyovyote lingewezekanaje? Mimi, na nikiwa mkongwe namna hii, nitapata raha tena, na bwana wangu pia.” Sasa angalia, hizo ni herufi ndogo za “mimi” pale, “bwana,” Ibrahimu. “Yeye akiwa mkongwe, pia.”

Ndipo Malaika akasema, “Kwa nini Sara akachekeka?” Loo, jamani!

214 Sasa, kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

215 Ni kitu gani? Ni Mungu, Roho Mtakatifu, akiishi miongoni mwa miili ya wanadamu, katika vyombo hivi vilivyowekwa wakfu ambavyo Damu ya Mwana wa Mungu imeviosa, kwa imani; na Mungu akiishi katika vyombo hivi, akifanya na kutenda kazi za Yesu Kristo, akimfanya yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama tumebatizwa na Roho Mtakatifu katika Mwili huo, basi tunakuwa Mwili wa Kristo. Ndipo tumefufuliwa pamoja Naye. Wakati Yeye alipofufuka, tulifufuka pia katika ufufuo pamoja Naye. Kwa sababu, Yeye ndiye Kichwa, nacho Kichwa pamoja na Mwili viko pamoja. Ndipo, leo, Kristo yuko ndani ya Kanisa, ndani yako, na kazi Zake ambazo alifanya wakati mmoja. Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi,

kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Hiyo ni kweli. Waebrania 13:8, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Unaona hapo?

²¹⁶ Watu hawatarajii hilo liwe hivyo. Wanatarajia sisi tuwe kundi la watu wajinga, wasiojua hata kile wanachozungumzia. Wanaamini kwamba ni kundi la mabwege. Lakini hu—huenda tukawa, kwa hali wanayozungumzia.

²¹⁷ Lakini tulimkubali Roho Mtakatifu jinsi Mungu alivyommimina, na tukapata matokeo yale yale waliyopata huko nyuma, kwa hiyo inathibitisha ya kwamba Yeye ndiye. Yeye ni Mungu asiyebadilika. Tunapata matokeo yale yale. Amina.

²¹⁸ Mama yangu mwenyewe wakati alipokuwa akifa, alisema, “Billy, umekuwa...” Nilimbatiza miaka mingi iliyopita. Akasema, “Kwa namna fulani umekuwa kiongozi wa mambo ya kiroho kwangu, Billy.”

Nikasema, “Mama...”

²¹⁹ Unajua, watu wetu ni Wakatoliki. Nami nikasema... Wakati nilipojua kwa mara ya kwanza ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu, nilijua jambo hilo maishani mwangu mwote, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, bali watu wangu kamwe hawakwenda kanisani. Ndipo nilishuka nikaenda na kuzungumza na kasisi, naye akasema, “*Hili* ndilo kanisa. *Hii* ndiyo njia.”

Nikasema, “Vema, Biblia? Ningeweza...?”

²²⁰ Kasema “Sasa, utachanganyikiwa kabisa. Unaona? *Hili* ndilo kanisa. Mungu yumo katika kanisa Lake. Huna budi kuliadini kanisa.”

²²¹ Vema, nilienda huko kwa Walutheri, nao wakasema, “Sisi ndio kanisa. Sisi ndio kundi la waaminio.”

²²² Nikaenda kwa Methodisti. Wakasema, “Sisi ndio kundi la waaminio.”

²²³ Nikaenda kwa Baptisti. Wakasema, “La, wote wamekosea. Sisi ndio hilo.”

²²⁴ Nikawazia, “Ni kitu gani kinachoendelea hapa? Kanisa ni kundi la watu. Na *hili* linasema *hivi*. *Hili* linasema *hivi*. Na *hivi*, na *vile*, na *vile*. Hapana budi kuna kasoro.”

²²⁵ Kwa hiyo nikasema, “Nilirudi moja kwa moja kwenye Biblia, mama, na kusoma jinsi hasa kanisa la kwanza lilivyofanya. Na jinsi walivyofanya jambo hilo, ndivyo nilivyolifanya, pia, ndipo nikapata matokeo yale yale.” Nikasema, “Mungu asifiwe. Hilo ni zuri vya kutosha kwangu.”

²²⁶ Mradi tu nilipata matokeo yale yale, ninamwona Yesu yeye yule. Ninamwona Mungu yeye yule aliyefanya kazi katika Agano la Kale, katika Agano Jipya, hata kwenye lile baraza la Nikea. Yeye alitenda kazi mle ndani mpaka kuja kwa kanisa Katoliki

la Kirumi lililokubali mafundisho ya sharti badala ya Biblia, likapitia katika nyakati za giza, kisha likarudi kupitia Luther, Wesley, na hapa chini katika wakati wa kanisa la Laodikia. “Na itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Mungu atalitoa Kanisa kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa. Kutakuwako. Na kuona Roho Mtakatifu yeye yule, kwa ahadi zile zile, akifanya kazi zile zile na jambo lile lile, Jina la Bwana na libarikiwe.

²²⁷ Mungu asiyebadilika atakupa Roho Mtakatifu yeye yule ambaye aliwapa kule, bila kigeugeu. Yeye atafanya mambo yale yale aliyofanya wakati alipokuwa hapa duniani, kwa mwanamume yeyote ama mwanamke yeyote atakayeliadini na kulikubali. Kama una Roho Mtakatifu, mshike kama vile Yakobo alivyofanya, na umshikilie mpaka matokeo dhahiri yaje. Amina. Liaminini, enyi marafiki.

²²⁸ Na kwenye wakati usiotarajiwa, na labda mahali pasipotarajiwa. Lakini kama Yeye atafanya jambo hilo katika mahali pasipotarajiwa, ni zaidi sana vipi Yeye atafanya hivyo usiku wa leo katika mahali panapotarajiwa, mahali tunapotarajia kuona jambo hilo likitukia?

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

²²⁹ Wakati vichwa vyenu vimeinamishwa, nami ninatumaini mioyo yenu imeinamishwa, pia. Samahani kwa kuwachelewesha kwa muda mrefu namna hii, mpaka saa tatu. Lakini ningetaka kuwauliza swali hili: Mwajua, huenda tusikutane tena. Huenda machweo yasije asubuhi kwa ajili ya wengine wetu. Na kama ingekuwa ni hivyo, kwamba kamwe hatutaona mapambazuko mengine, je! tungekutana tena ng'ambo ya mto? Je! kungekuwako... Je! una ile amani na ninii... moyoni mwako, na hakikisho, hakikisho la Kimaandiko kama watu hawa nilionena habari zao usiku wa leo, ya kwamba ulipokutana na Mungu, ulipata tukio la Kimaandiko? Mungu aliyabadilisha maisha yako kabisa, na sasa wewe si mtu yule yule, aliyejengwa tu upya, akapigwa msasa, bali wewe ni kiumbe kipya, kiumbe kipya katika Kristo? Kama sivyo ulivyo...

²³⁰ Hatuna pa kusimama madhabahuni, ama nafasi. Lakini ningetaka kuomba uaminifu wenu. Kama mngetaka ya kwamba niwaombee hapa, kutoka mimbarani, tukijua ya kwamba siku moja itanibidi kukutana nanyi tena na kukutana na maneno yangu niliyosema usiku wa leo, je! mngeninii, kwa... wote wakiwa wameinamisha vichwa vyao na kufunga macho yao, je! ungeinua tu mkono wako na kuonyesha, kwa huo, “Niombe, ndugu, kwamba ni—ninataka kuwa namna hiyo?”

²³¹ Mungu akubariki, na akubariki. Akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki. Nje, mahali popote, wekeni mikono yenu kuegemea madirisha, popote pale. Mungu atabariki.

²³² Inua tu mkono wako, katika uaminifu wa kina, na useme, “Mungu, nirehemu. Da—daima nimetaka kuwa hivyo, Ndugu

Branham, lakini kwa njia moja ama nyingine, kamwe sijawahi kupata jambo hilo.”

²³³ Loo, ewe rafiki mpendwa, je! hutashikilia jambo fulani? Niamini mimi, kama mtumishi Wake. Roho Mtakatifu ni wa kweli. Usimruhusu mtu yeyote kukushawishi ukamwache Yeye. Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika, ewe rafiki Mkristo. Kama ndio kwanza ujiunge na kanisa, kama ndio kwanza ubatizwe katika maji, wala bado hujabatizwa kwa Roho Mtakatifu, kwa kweli hujaongoka bado.

²³⁴ Sasa, unasema, “Ndugu Branham, ni—nilinena kwa lugha, ni—nilifanya *hivi*, ama nilifanya *vile*.” Sasa, ninaamini katika jambo hilo pia. Niliwaambia. Lakini, kumbukeni, ungeweza kucheza katika Roho. Ungeweza kunena kwa lugha.

²³⁵ Nimewaona Wahindu wakifanya hivyo. Nimewaona wachawi wakinena kwa lugha, wakaifasiri. Nami nimesikia. Nilienda kwenye kambi moja wakati mmoja, ambako kulikuwako na ndugu fulani waliokwenda kule, nami nikaona meza ikigongagonga katika lugha, na penseli ikaja na kuandika katika lugha zisizojulikana; kisha wakayasoma. Unaona? Mambo hayo yote, hiyo ni, huyo angeweza kuwa ni Ibilisi.

²³⁶ Lakini, ndugu, kama unanena kwa lugha, halafu uendelee kuishi maisha uliyoishi huko nyuma, basi tukio lako lina kasoro fulani. Unaona? Kama una hicho, kitu pekee unachoegemea ni kunena kwa lugha, kamwe usijaribu jambo hilo. Utaanguka kwenye maporomoko, wala mtumbwi huo kamwe hautayastahimili. Lakini kwa ninii . . .

²³⁷ “Zikiwapo lugha zitakoma. Ukiwapo unabii, utabatilika. Lakini ijapo ile iliyo kamili,” loo, ule upendo wa Mungu, tajiri sana tena safi, usiopimika na wenye nguvu, ndipo karama hizi zingine zitatenda kazi vizuri pamoja nao. Unaona? Hizo ni karama za Roho Mtakatifu ulizopewa, kunena kwa lugha, kutabiri, na chochote kile, kufasiri. Hizo ni kwa ajili ya kulijenga Kanisa, kwa ajili ya kuujenga ule Mwili. Lakini kwanza mpokee Roho Mtakatifu, hivi kwamba uone kwamba maisha yako yamebadilika.

²³⁸ Sasa, kumekuwako na mikono minane ama kumi iliyoinuliwa tangu nimekuwa nikizungumza. Je! kungekuwako na mwingine kabla sijafanya maombi? Mungu akubariki, mama. Vema, Mungu akubariki, dada. Kungekuwako na mtu mwingine? Inua tu mkono wako, useme, kwa uaminifu wa kina, “Ndugu Branham, nikumbuke.” Mungu akubariki pale, ndugu. Mtu mwingine? Sema tu, “Niombee.” Ninaweza tu kukuombea, rafiki yangu. Mungu akubariki, mama. Na Mungu akubariki pale, dada. Sasa, Yeye anauona mkono wako.

²³⁹ Kumbuka, Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye maneno yangu, anayeamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia

Uzimani.” Hatuna budi kuamini jambo hilo kwa moyo wetu wote. Liamini tu kwa yote yaliyo ndani yako, naye Mungu atashughulikia hayo mengine.

²⁴⁰ Baba wa Mbinguni, sasa tunakupa wasikilizaji hawa wachache. Maneno haya yaliyovunjikavunjika, yaliyonenwa kwa wasiwasi usiku wa leo, Bwana, nikisimama hapa nikiwahurumia watu hao waliosimama pale, na viungo vyao vikiuma. Mungu, nadai nafsi yao. Vizuri sana nijuavyo, Bwana, kulileta Neno, kwa njia yangu maskini nyenyekevu, mbegu yoyote ndogo iliyokuwa ndani yake, Baba, ipande mioyoni mwa watu hao. Nami ninadai nafsi yao, kwamba haitapotea, bali itatokea huko ng’ambo katika siku ile katika ule ufufuo. Tujalie, Bwana.

²⁴¹ Wewe ni Mungu. Hakuna Mungu mwingine ila Wewe. Makafiri wana sanamu. Sisi tuna Mungu aliye hai, Mungu pekee aliye hai. Tungeweza kuwazia juu Yako, Baba, ukiketi huko ng’ambo katika Umilele, mara milioni ukiwaka zaidi ya majua bilioni kumi. Ee Mungu, angaza! Wewe ambaye ungeweza kuziumba dunia, ukaweka ule mfumo mkuu wa jua mbinguni, kisha—kisha ukashuka ukaja kumwoko mwenye dhambi, ukahusika vya kutosha kuwa hapa katika maskani hii ndogo usiku wa leo pamoja na watu hawa Wakristo. Kwa kuwa, Yesu alitupa Neno, ya kwamba, “Popote wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa kati yao.”

²⁴² Sasa, waokoe hawa watu, Baba. Hayo tu ndiyo ninayojua kukuomba, nami ninaamini ya kwamba utayajibu maombi yangu. Nami ninaomba ya kwamba kesho watakuwa moja kwa moja kanisani, na wakiwa tayari kwa ajili ya ubatizo, hata leo usiku pia, kama hawajapata kubatizwa. Ninaomba ya kwamba Wewe utawajaza kwa Roho Mtakatifu. Jalia washikilie Kweli hii halisi ya Mungu mpaka mauti yatakapowaweka huru. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

²⁴³ Sasa, wasikilizaji, ninataka kuwauliza swali moja, kwa uchaji, kwa heshima sana. Katika dakika chache tutafunga. Kama nilvyosema, huenda tusikutane tena. Ninatumaini tutakutana. Lakini kumbukeni, itatubidi kutoa hesabu kwa ajili ya usiku wa leo, tutakapokuja Hukumuni. Itanibidi kutoa hesabu kwa yale nimesema, kwa yale ninafanya. Itabidi yote yatolewe hesabu, kwa Mungu. Na kama—kama nikipatikana na hatia, mnajua litakalonipata. Afadhali uniache nife mwenye dhambi, bali usiniache kamwe nife mdanganyifu. Jalia niwe mkweli, mwaminifu.

²⁴⁴ Sasa, angalieni. Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele...Nami ninaomba jambo hili. Sasa, sijui kama atafanya hivyo. Maana, hili ni kundi dogo tu la wasikilizaji...Na kuna watu wanaosimama, na wakati umekwishia. Nimewachelewesha kupita kiasi. Linge kuwa ni

jambo gumu kufanyiza mstari wa maombi kupitia hapa, lakini nitawaombea katika wasikilizaji. Lakini hebu... Ninaomba ya kwamba Mungu atawapa jambo fulani ambalo mnaweza kushikilia kwa mikono yenu, kama vile Yakobo alivyofanya; hamjapata kuwa nalo, mnaona, jambo fulani mnaloweza kushika kwa mikono.

²⁴⁵ Sasa, ninyi watu huko nje mnaoteseka, nilizungumza nanyi kuhusu Malaika aliyeshuka, ambaye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, ambaye amedhihirishwa ndani yetu kama sisi ni waaminio. Halafu alipokuwa ameelekeza mgongo wake, Sara... Yeye alifahamu yale Sara aliyokuwa akisema na kufanya katika wasikilizaji.

²⁴⁶ Ndipo wakati mmoja, kulifanya dhahiri kwenu, kwamba alipitia kwenye u—umati wa watu, na kulikuwako na maskini mwanamke mdogo ambaye labda angevunjika moyo tu kama mtu mwingine yeyote hapa.

²⁴⁷ Kwa kawaida sisi... Jana usiku tuliingia kwenye vurugu ndogo. Nasi tulikuwa na watu wengi sana wa kuombewa, tulinwagiza yule mvulana kutoka aende akagawe kadi za maombi wakati nilikuwa bado ninahubiri. Na kwa hiyo wakati mwingine wanakuja na kurudi, na kuja na kurudi. Nanyi nyote mnataka kwenda kwenye shule ya Jumapili. Mtu fulani aliniambia huko nje, kasema, “Waachilie watoke mapema, maana watu hawa hawana budi kuendesha magari mbali na kurudi kwa ajili ya shule ya Jumapili.”

²⁴⁸ Ninataka kutimiza ahadi hiyo. Nilisema, “Nitafanya hivyo. Nitalifanya.” Mnaona? Nami ni—ninawataka mtulie. Kama...

²⁴⁹ Jambo muhimu, ni, kukamata kitu fulani kilicho halisi. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁵⁰ Basi, kama—kama niliwaambia roho ya John Dillinger ilikuwa imekuja juu yangu, ningekuwa mtu hatari wa kukaribiwa. Ningekuwa na bunduki na kuwa haramia. Kama niliwaambia roho ya—ya mwanasanaa fulani mashuhuri ilikuwa juu yangu, mngenitarajia kuchora picha kama mwanasanaa huyo angaliweza kuchora. Kama niliwaambia roho ya—ya—ya Houdini, yule mwanasanaa mtoro, mnetarajia nifanye mambo aliyofanya. Kama niliwaambia roho ya mwanamuziki fulani mashuhuri ilikuwa juu yangu, mnetarajia niguse vibao hivyo kwa njia fulani tu, kwa kuwa roho yake iko juu yangu. Unaona?

²⁵¹ Kama nikiwaambia Roho wa Kristo yuko juu yangu, basi fanya kazi za Kristo. Kristo alisema ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Sote tunajua hivyo, ya kwamba Mungu alijiwakilisha Mwenyewe katika Kristo, kuupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Yeye alikuwa Imanueli. Yesu

alisema, “Si Mimi ninayefanya hizo kazi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu, Yeye hufanya hizo kazi.”

²⁵² Na wakati akipita, akiwa na Roho yuyo huyo ndani Yake, maskini mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi Lake. Sasa, Yeye hakuhisi hilo, kimwili. Mnajua kamwe hakuhisi. Hakika hakuhisi. Maana, vazi la Kipalestina, kama mtu yeyote anajua, lilikuwa na nguo ya ndani, na vazi kubwa linalopwaya chini namna *hiyo*. Kwa hiyo kamwe Yeye asingegusa . . . Angeninii . . . Mwanamke huyo kamwe asingekuwa . . . Kamwe asingehisi hilo, na kila mtu akiwa amemzunguka. Lakini aligusa vazi Lake kwa imani.

²⁵³ Kipofu Bartimayo aligusa vazi Lake siku moja, langoni, kwa maana kamwe asingaliweza kusikia kilio hicho.

²⁵⁴ Baadhi yao wakisema, “Aisee, Wewe, unafufua wafu. Kuna uwanja mzima wa makaburi uliojaa hao huku nje. Njoo, fanya hivyo,” na kumdhihaki. Na makuhani na kila kitu, “Njoo, ufanye *hivi*, na ufanye *vile*.” Kamwe Yeye hakusema neno.

Lakini mwombaji kipofu, “Ee Mungu!”

Ndipo Yesu akasimama. “Mleteni hapa.” Unaona? Unaona?

²⁵⁵ Maskini mwanamke huyo aliona asingeweza kamwe kupata usikivu wake, kwa maana marabi na makuhani na kila mtu alikuwa amemzunguka, na kila mtu. Naye akagusa vazi Lake. Ndipo Yesu akasimama, kasema, “Ni nani aliyenigusa?”

²⁵⁶ Na Petro hata alimkemea, akasema, “Ati ni nani ‘aliyekugusa’ Wewe? Kila mtu anakugusa. Kwa nini useme jambo kama hilo?”

²⁵⁷ Akasema, “Lakini naona kwamba uwezo, nguvu zimenitoka. Mtu fulani alikuwa na mguso fulani.”

²⁵⁸ Ndipo akaangalia kote katika wasikilizaji mpaka akampata maskini mwanamke huyo. Na shida yake ilikuwa ni nini? Alikuwa akitokwa na damu. Na kama alikuwa na imani ya kutosha kumgusa Mungu, hilo lilisababisha hisia kwa Yesu. Ndipo kama Kristo yumo ndani yetu, ukiwa umetiwa mafuta na Roho Mtakatifu, hivi shauku yako si itagusa kitu kile kile?

²⁵⁹ Sasa, ninataka kuwaulizeni ninyi wahudumu jambo fulani. Biblia si inasema, ya kwamba, “Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu”? Hiyo ni kweli? [Wahudumu wanasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ni wangapi wanaojua jambo hilo kwamba ni kweli? [“Amina.”] Biblia ilisema hivyo, Agano Jipya. “Yeye sasa hivi ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika” nini “mambo yetu ya udhaifu.”

²⁶⁰ Vema, basi, ungejua ya kwamba ulimgusa? Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye atatenda vile vile alivyotenda jana. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁶¹ Vema, sasa, Yeye hana mikono duniani bali yangu na yako. Sauti Yake duniani ni yetu; sauti yetu imetolewa Kwake. Hiyo ndiyo sababu tunahubiri Injili. Tunaamini sio sisi. Tunavuviwa kuhubiri mambo hayo, Roho Mtakatifu akinena kupitia kwetu. Unaona? Hatuamini sisi ndio tunaoweza kufanya jambo hilo. La hasha. Ninajua mimi nisingeweza. Na—nasi—tunajua ya kwamba ni uvuvio wa Roho Mtakatifu.

²⁶² Basi kama mtu akihubiri jambo fulani ambalo ni kinyume, anakana Neno; basi Roho Mtakatifu anawezaje kuliandika Neno, kisha ageuke, alighairi kupitia kwa mwanadamu? Hawezi kufanya hivyo. Inabidi iwe ni Neno. Halina budi kutokea jinsi tu lilivyoandikwa, vivyo hivyo hasa.

²⁶³ Sasa, kama “Yeye ni Kuhani Mkuu.” Hebu tushikilie Andiko hilo moja, tuchukue hilo tu. Kama Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, basi njia pekee ungaliweza kujua, Yeye angeninii... Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye atafanya vile vile alivyofanya hasa wakati mwanamke huyo alipomgusa.

²⁶⁴ Ndipo basi kama mimi ni mtumishi Wake, na Roho Wake yumo ndani yangu, unaweza kugusa vazi Lake popote ulipo. Lisingeninii...

²⁶⁵ Vazi langu lisingelela tofauti yoyote. Mimi ni mwanadamu, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Lakini si zaidi ya mke wako, mume wako, ama ndugu, yeyote yule angekuwa, mchungaji wako. Sisi sote, sisi ni sawa. Lakini Yeye ndiye Kuhani Mkuu. Mimi si Kuhani Mkuu. Yeye Ndiye.

²⁶⁶ Wewe ukinigusa haitakufaa kitu; bali kumgusa Yeye kutafaa. Lakini kama ninaweza kujitoa Kwake... Mimi ni kama tu hii—hii maikrofoni hapa. Maikrofoni hii ni bubu kabisa mpaka kitu fulani kizungumze ndani yake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.]

²⁶⁷ Vema, basi, simjui mmoja wenu huko nje. Na kama nikimwona Yeye juu ya baadhi yenu ninaowajua, nisingesema jambo lolote. Ninamjua Ndugu na Dada Dauch wanaoketi moja kwa moja pale. Nami ninaamini huyu ni maskini yule ndugu Mgiriki hapa kutoka Ugiriki ambaye si—ambaye siwezi kukumbuka jina lake, David. Na nje ya hao, nafikiri huyu ni nanii... watu hawa papa hapa, naam, hawa wasichana watatu ama wanne papa hapa kwenye safu hii ya mbele, ninawajua, maana wametoka Georgia na huko Tennessee. Wanahudhuria kanisa langu. Baadhi ya watu hao wanaendesha magari maili elfu moja mia tano Jumapili, kila Jumapili ninayohubiri. Nje ya hao, nafikiri Dada Evans anaketi moja kwa moja pale, na Dada Ungren na hao wengine, Ndugu Evans, anayeketi moja kwa moja hapo.

268 Sasa ninawaulizeni ninyi watu. Ni wangapi hapa ndani ambao ni wagonjwa, nao wanajua ya kwamba mimi siwajui, sijui lolote kuwahusu? Inueni mikono yenu. Iweni na imani.

269 Sasa, Baba wa Mbinguni, unajua moyo wangu. Nami siji huku, kufanya maonyesho jukwaani, ya Wewe Bwana. Haikulazimu kufanya jambo hili. Kama hutaki kulifanya, Baba, haliko kwenye mapenzi Yako ya Kiungu, basi lifunge tu, kwa ajili yao. Tunajisikia ya kwamba Roho Mtakatifu amekuwa hapa na akatubariki.

270 Lakini kwa kuwa nilizungumza juu ya somo hilo, “Mimi ni Mungu, wala sina kigeugeu.” Basi wakati ulipotembea hapa katika umbo la kibinadamu, duniani, Imanueli, maskini mwanamke mmoja aligusa vazi siku moja, naye alikuwa na imani kubwa sana hivi kwamba Yeye aliihisi. Nalo Neno Lako linasema, Baba, ya kwamba, usiku wa leo, ya kwamba Yesu, Mwanao, ni Kuhani wetu Mkuu, Naye angali anaweza kuchukuana na hali yetu ya udhaifu.

271 Wako wale humu ndani ambao ni wagonjwa. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawaruhusu, angalau mmoja ama wawili, ama wowote wale humu ndani, Bwana, kusudi watu wapate kitu cha kushikilia, kama vile Yakobo, na kujua ya kwamba ni Roho Mtakatifu, wala wasimwachilie mpaka watakapobarikiwa. Jalia, kama tu utafanya jambo hilo, Bwana, kila mgonjwa hapa ndani aishike ahadi hiyo hiyo, na adumu nayo mpaka watakapohakikishiwa moyoni mwao ya kwamba baraka za Mungu zinakaa juu yao.

272 Sasa, ninawakabidhi wasikilizaji hawa Kwako, Ujumbe pamoja na mimi mwenyewe, kwa ajili ya kazi Zako. Ni zaidi ya yale ninayoweza kufanya, ama mtu mwingine yeyote anavyoweza kufanya, tangu sasa na kuendelea, Bwana. Inabidi iwe ni Wewe, kwa hiyo jithibitishe kwamba Wewe upo, yeye yule jana, leo, na hata milele, Mungu asiyebadilika. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba jambo hili. Amina.

273 Sihisi Roho Wake, mnaona, kwa njia hiyo. Ni karama. Hiyo haimaanishi ni Roho Mtakatifu zaidi ya vile mtoto mdogo angekuwa naye. Ni karama tu inayoambatana na Roho Mtakatifu, kulifanya Neno liishi. Sasa, hili, msiwe na ninii... Kama Yeye angefanya jambo hilo, haiwabidi kuhofu. Ni—ni Neno lililodhihirishwa. Ni Neno lililodhihirishwa.

274 Sasa, ninataka tu kila mmoja wenu enyi watu kuwazia jambo hili moyoni mwenu. Ninii tu—wazieni tu jambo hili. Haikubidi kuomba kwa sauti kuu. Jiombee tu mwenyewe moyoni. “Bwana, nina hakika Ndugu Branham hajui lolote juu yangu. Hajui ugonjwa wangu. Hajui lolote kunihusu mimi. Wala sijaribu kumgusa mhudumu huyo. Lakini yeye ametwambia kwa udhahiri sana ya kwamba Wewe ulikuwa ni Kuhani Mkuu, nami nimesoma jambo hilo. Na ninakuomba,

hebu jalia tu aseme nami, kama vile Yesu alivyosema na yule mwanamke pale... ambaye aligusa vazi Lake. Na ninii tu... ”

²⁷⁵ Ama, kama wewe si mgonjwa, useme, “Bwana Yesu, jalia... Daima nimekuwa kidogo nikishuku jambo hili, lolote la kimbinguni. Lakini kweli ningetaka kuwa na kitu fulani ningaliweza kukishika kwa mkono wangu. Kwa hiyo jalia aseme na *Fulani wa fulani* hapa ndani. Ninamwombea mwanamume ama mwanamke. Jalia—jalia aseme hivyo. Nitaamini.” Itakuondolea yote. Hilo litakuwa ni jambo unaloweza kushika kwa mkono wako, kama vile Yakobo, na kusema, “Hili ndilo lenyewe.” Yeye alimshika Mungu, wakati mmoja, na kusema, “Mimi hapa. Ninaweza kulishika.”

²⁷⁶ Je! lingewafanya ninyi nyote kuamini? Kama ungeamini, inua mkono wako. Useme, “Ninii tu—zidisha tu imani ndani yangu,” kila mahali, “laiti ningaliweza kuliona likifanywa.” Mungu awabariki.

Sisemi ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo. Ninatumaini ya kwamba atafanya.

²⁷⁷ Wakati mmoja, alipokuwa akishuka mlimani, Yeye alisema, “Mambo yote yanawezekana, kama tu unaweza kuamini,” akimwambia baba wa yule mvulana mwenye kifafa. Laiti tungaliweza kuamini tu! Mtu aliye mgonjwa na ni mhitaji, amini. Amini kwa moyo wako wote. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

“Ati unasema unangojea nini, Ndugu Branham?”

²⁷⁸ Kila mmoja humu ndani, hapana shaka, nimekuwa Phoenix mara nyingi sana, mmeiona, kuhubiri ujumbe namna hii. Lakini, ni Nuru. Wana picha Yake. Yeyote, karibu ninyi nyote, mmeona Nuru hiyo. Sivyoy? Mnayo kwenye picha na kadhalika. Ambapo, iko Washington, D.C. Waliipiga picha tena hapa, hivi majuzi. Unaona? Hiyo inajishuhudia Yenyewe, ni Nguzo ya moto iliyowaongoza wana wa Israeli nyikani.

²⁷⁹ Hiyo Nguzo ya moto ilifanyika mwili na kukaa kwetu. Yesu alisema, “Nilitoka kwa Mungu, Nami ninaenda kwa Mungu.” Baada ya kufufuka Kwake Yeye alipaa Juu.

²⁸⁰ Na alipofanya hivyo, alikutana na Paulo akienda zake Dameski, Naye alikuwa amerudi akawa Nuru tena. Paulo angeweza kuiona. Hao wengine wasingeweza kuiona. Hata ilimpofusha. Alikuwa kipofu. Naye alisema aliona Nuru hii hapo, ikiangaza kama jua. Akasema, “Bwana, U Nani Wewe?”

²⁸¹ Akasema, “Mimi ni Yesu. Na ni vigumu kwako kupiga teke mchokoo.”

²⁸² Sasa, Nuru ile ile, picha Yake, kama hiyo ndiyo Nuru ile, kama hiyo ni Nguzo ile ile ya Moto, Yesu yeye yule aliyekuwa katika njia ya kwenda Dameski, Paulo, itafanya kazi zile zile. Haina budi kufanya.

283 Hii hapa. Bwana asifiwe. Asante, Bwana Yesu. Sasa hebu Shetani ajaribu kusema jambo fulani!

284 Maskini mama huyu anayeketi hapa akiwa na nguo ya bluu, akiwa na ugonjwa wa uvimbe wa pua, akiomba, amini kwa moyo wako wote na utakuacha. Utaiamini? Vema basi, unaweza kupokea. Sijapata kumwona mwanamke huyo, sijapata kumwona maishani mwangu. Mambo hayo ni kweli, sivyo, mama? Yakiwa ni kweli, inua mkono wako, upunge. [Huyo dada anasema, “Ni ya kweli.”—Mh.] Ulikuwa ukiomba kuhusu jambo hilo, “Bwana, mjalie aninii. . .” Uwe na imani.

285 Huyu hapa maskini mama mzuri ameketi, ameketi papa hapa nyuma, amevaa koti la manyoya ama kitu fulani. Hiyo hapo ile Nuru. Hivi hamwezi kuiona imening’inia juu ya yule mwanamke pale? Mwanamke huyo yuko katika hali mbaya. Simjui, sijapata kumwona maishani mwangu.

286 Kama hatufahamiani, inua mkono wako. Lakini, sikiliza. Jambo hili si ni kweli, hisi ya ajabu kweli imekuzunguka, tamu sana, hisi nyenyekevu? Hiyo ni ile Nuru. Ninaiangalia moja kwa moja. Hapa. Una uvimbe. Si uvimbe tu, bali vivimbe. Viko kila mahali mwilini mwako. Hiyo ni kweli. Sivyo? Unaamini? Mungu akuponye na akufanye mzima. Iweni na imani.

Mnaamini?

287 Hapa, maskini mama mmoja aliinua mkono wake, papa *hapa* nyuma, anaketi nyuma ya mtoto huyu, katika kiti cha magurudumu. Simjui mama huyo. Sijapata kumwona. Hatufahamiani. Sivyo, mama? Lakini unaomba kwa ajili ya ugonjwa wa moyo, kwamba Mungu atakuponya. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako namna *hii*. Yesu alikuponya. Nenda nyumbani ukawe mzima.

288 Je! mnaamini kwa moyo wenu wote sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Kama mnaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Iweni na imani. Msitilie shaka. Aminini tu kwa ninii yote. . .

289 Huyu hapa mwanamke ameketi moja kwa moja *hapa*, ameketi moja kwa moja chini, wanawake kadhaa kutoka kwa Bi. Sharritt. Ameketi pale, akiomba. Ana yabisi kavu. Amini jambo hilo, mama. Unaliamini? Vema. Pokea.

290 “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Biblia ilisema itakuwa. Mungu asiyebadilika!

291 Niambieni walimgusa nani. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mimi, kwa uchaji, huku nimeinua mikono yote miwili, sijapata kuwaona watu hao hapo kabla, sijui lolote kuwahusu. Lakini Yeye ambaye yupo sasa, usingeweza kuyaficha maisha yako hata ufanye nini. Hiyo ni kweli. Yeye yupo hapa. Yeye ni Kristo. Ni halisi. Ni ahadi Yake, Mungu yeye

yule. Hivi huwezi kuishika? Inyakue na kusema, “Ni yangu. Sasa ninaamini.”

²⁹² Baba wa Mbinguni, ninawaleta wasikilizaji hawa Kwako, watu hawa wagonjwa. Ni wahitaji. Kama tulivyonukuu jana usiku, kulikuwako na maskini mchungaji mmoja wa kondoo wakati mmoja, jina lake Daudi. Alipewa jukumu, kuwachunga kondoo wa baba yake. Kuna wachungaji wengi wanaoketi hapa usiku wa leo, pia, Bwana. Wala hakuwa na vitu vingi vya kujihami, na kuwalinda kondoo, ila kombeo tu. Hilo lilitosha. Siku moja simba aliingia na kumshika mmoja wa kondoo wake, akamnyakua. Daudi alijua ya kwamba Mungu wa Mbinguni alikuwa pamoja naye, naye akanyakua kombeo hili na kumfuata huyo kondoo. Ndipo akamwua huyo simba, akamwangusha kwa kombeo hilo, na kumrudisha huyo kondoo angali hai.

²⁹³ Baba, ugonjwa, ibilisi, zaidi ya simba, amewashika wengi wa kondoo Wako. Nina kombeo dogo hapa; linaitwa maombi na imani. Halionekani kana kwamba linafaa kitu, ukilinganisha na zana za vita za sayansi ya tiba. Lakini, Mungu, Wewe lielekeze ombi hili mahali pale.

²⁹⁴ Ewe Shetani, waachilie. Ninamfuata huyo kondoo. Waachilie. Ninawarudisha kwenye malisho ya Baba tena usiku wa leo.

²⁹⁵ Katika Jina la Yesu Kristo, ninamkemea kila ibilisi wa magonjwa, nikiyatoa ndani ya watu hawa. Na jalia waondoke, wakiwa huru, tangu wakati huu na kuendelea, kupitia Jina la Bwana Yesu Kristo.

²⁹⁶ Nyote mnaoamini uponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu, na kusema, “Sasa ninakubali uponyaji wangu. Ninaweka mikono yangu juu ya Huyu, huyo ni Kristo, na ninaamini kwa moyo wangu wote.”

Mchungaji wenu.



MUNGU ASIYEBADILIKA AKITENDA KAZI
KATIKA NJIA ISİYOTARAJIWA SWA62-0120

(The Unchangeable God Working In An Unexpected Way)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrión Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 20 Januari, 1962, katika Westwood Assembly Of God huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org